*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

# Uelekeo

## Trump kutoka kwenye majengo hadi siasa






Uk. 17

| ISSN 2953-2787 | Toleo Na. 00086 | Bei Tanzania sh 1,000 | Jumatano Oktoba 23 - 29, 2024 |

### "Tumejipanga, tupo tayari jukumu la uangalizi"

Uk. 3



### Je; ulaji wa mkate una athari za kiafya mwilini?

Uk. 7



### Tusichague viongozi alimradi, tuwe na vigezo hivi:

Uk. 12



# Pochi la Mama Samia lafunguka

- Bil. 97.1/- kujenga Daraja la Jangwani



## Dk. Slaa awaumbua viongozi wa Chadema

Uk.4



## 8 wafa, 39 wajeruhiwa ajali ya mabasi







Uk. 3

rifaly

Habarika kidijitali! Soma gazeti la Uelekeo ndani ya Rifaly!



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com

# Tz, Singapore kubadilishana uzoefu katika sekta ya nishati

**Na Mwandishi Maalum, Singapore**



NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amesema Tanzania na Singapore, zitaenzi uhusiano uliopo, kuongeza biashara na kubadilishana uzoefu katika sekta ya nishati.

Alisema hayo juzi baada ya kukutana na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Viwanda na Biashara wa Singapore, Gan Kim Yong.

"Tunatakiwa kujifunza kutokana na uhusiano huu na hasa kutoka Singapore kwa kuwa mmepiga hatua katika sekta ya nishati hadi kuwa na uwezo wa kufikia mahitaji ya juu ya umeme ya zaidi ya Gigawati nane, hicho ni kiasi kikubwa ikilinganishwa na Tanzania yenye takribani Megawati 3,000 ambapo hadi mwaka 2030, tumepanga kufikia Megawati 10,000.

"Mpango huo hauwezi kutokea bila kuwa na ushirikiano na wadau na nchi nyingine kama Singapore, ni matumaini yetu kuona ushirikiano huu unaendelea kukua kati ya nchi zetu na kuleta manufaa kwa wananchi," alisema.

Aliipongeza Singapore kwa uzalishaji wa umeme wa jua na kusema kuwa Tanzania inaendelea na jitihada zake za kuzalisha umeme huo.

Akitaja miradi ya nishati inayoendelea kutekelezwa, Dk. Biteko alisema kuwa kwa sasa nchi inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha megawati 2,115.

Aidha, upembuzi yakinifu unaendelea kuhusu miradi mbalimbali ya uzalishaji umeme.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Mkuu Dk. Biteko, alimualika Naibu Waziri Mkuu wa Singapore, Yong nchini Tanzania.

"Kwa niaba ya Serikali na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, tutafurahi ukija Tanzania na tunaamini kuna maeneo mengi ya kushirikiana nanyi," alisema.

Kwa upande wake, Naibu Waziri Mkuu wa Singapore, Yong alisema nchi yake ipo tayari kuendelea kushirikiana na Tanzania na kuwa nchi hizo zina mahitaji yanayofanana.

Aidha, alisema Singapore inatumia zaidi gesi asilia kama chanzo cha nishati ingawa pia inatumia umeme unaozalishwa kwa maji, jua na upepo.

Vilevile, alisema nchi yake iko tayari kushirikiana na Tanzania katika kubadilishana uzoefu kwa masuala mbalimbali yanayohusu sekta ya nishati.

# Camartec yasambaza mashine kwa wakulima walioko vijijini

**Na Mwandishi Wetu, Karatu**

MKUU wa Wilaya ya Karatu, Dadi Kolimba, amekipongeza Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC) kwa kusambaza teknolojia na mashine mbalimbali za kulima, kuvuna na kuchakata mazao pamoja na kuyaongezea thamani.

Alisema hayo baada ya kutembelea kituo kihandisi cha Teknolojia za Kilimo kilichoanzishwa na CAMARTEC katika Kijiji cha Gongali juzi.

Katika kituo hicho, alijionea zana mbalimbali ikiwemo mashine za kupukuchua mahindi, maharage, alizeti na matrekta.

Alisema kituo hicho kitawasaidia wakulima kulima kwa kisasa na kuchakata mazao yao kwa kutumia zana za kisasa.




Aliipongeza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuiwezesha Camartec kufungua kituo kijijini hapo na kuwafikia wakulima wengi na kuongeza kuwa uhitaji wa mashine hizo bado ni mkubwa kwa wilaya hiyo yenye wakulima wengi zaidi.

Kaimu Mkurugenzi wa CARMATEC Mhandisi Godfrey Mwinama, alisema wataendelea kufanya utafiti na kutengeneza mashine ambazo zitakuwa mkombozi kwa wakulima kwa kuwaokolea muda na gharama walizokuwa wakitumia kutokana na teknolojia duni.

"Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kutuwezesha kuwasogezea wakulima wa vijijini mashine mbalimbali," alisema.

Baadhi ya wakulima waliokuwepo kituoni hapo, Rogati Israel na Mussa Hussein, walisema mashine walizozipata kutoka CAMARTEC, zimewasaidia kupukuchua mahindi na maharage kwa muda mfupi bila kuharibu ubora wa mazao hayo.

# Dk. Samia atuma salamu za rambirambi kwa Mwamposa



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan, amemtumia salamu za rambirambi Mchungaji Boniface Mwamposa kufuatia kifo cha Msaidizi wake Mkuu Jonathan Togolai.

Alituma salamu hizo kupitia akaunti yake rasmi ya Instagram jana.

Rais Dk. Samia alisema: "Nifikishie pia salamu zangu za pole kwa waumini wa Kanisa la Inuka Uangaze, familia, ndugu, jamaa na marafiki kwa kuondokewa na ndugu yetu huyu."

Alisema anawaombea utulivu, tafakari na shukrani kwa Mwenyezi Mungu katika kila jambo, kama inavyosomwa kwenye Biblia Takatifu, Kitabu cha Ayubu 1:21.



Marehemu Jonathan Togolai

Mchungaji Boniface Mwamposa

# Pinda: Tumejipanga, tupo tayari jukumu la uangalizi




**Na Mwandishi Maalum, Gaborone**

MKUU wa Misheni ya Uangalizi wa Uchaguzi ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC-SEOM), Mizengo Pinda, amesema wamejipanga na wako tayari kutekeleza jukumu la uangalizi kwa ukamilifu kama walivyoaminiwa na Jumuiya na kuwatuma kuifanya kwa niaba yao.

Alisema hayo alipokutana na Mabalozi kutoka nchi za SADC wanaoziwakilisha nchi zao nchini Botswana katika kikao kilichofanyika jijini Gaborone juzi.

Akizungumza katika kikao hicho, Pinda ambaye ni Waziri Mkuu mstaafu, alisema juzi kuwa amewaarifu Mabalozi hao juu ya uwepo wake kama Mkuu wa Misheni ya Uangalizi ya Uchaguzi ya SADC pamoja na waangalizi wengine kutoka nchi wanachama wa SADC.

Alisema amekutana nao ikiwa ni sehemu ya ratiba zake mbalimbali ili kuwasiliana nao moja kwa moja na hivyo kusaidia waangalizi kupata picha halisi ya jinsi maandalizi ya uchaguzi huo kwa ujumla yanavyokwenda.

Alisema wao kama viongozi wa SEOM, watakuwa na mikutano na watu mbalimbali ikiwa ni sehemu ya kusikiliza na kupata maoni ili kuhakikisha kazi yao ya uangalizi inakwenda vizuri

Akizungumza kwa niaba ya Mabalozi hao, Balozi wa Jamhuri ya Angola na Mkuu wa Mabalozi wa SADC nchini Botswana, Beatriz Morais, alishukuru kukutana na uongozi wa SEOM na kuahidi kushirikiana nao ili kuhakikisha kazi yao ya uangalizi inafanyika kwa mafanikio na hivyo kuleta tija na ufanisi kwa Jumuiya na nchi inayohusika.

# 8 wafa, 39 wajeruhiwa mabasi yakigongana

**Na Mwandishi Wetu, Mwanza**

WATU wanane wamefariki dunia na wengine 39 kujeruhiwa baada ya mabasi waliyokuwa wakisafiria kugongana uso kwa uso eneo la Ukiliguru Wilaya ya Misungwi mkoani Mwanza.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo jana alfajiri.

Alisema ajali hiyo ilitokea baada ya basi la Asante Rabi lenye namba za usajili T458 DYD lililokuwa likitokea Mwanza kuelekea Arusha kujaribu kulipita basi la Nyehunge lililokuwa likitokea Morogoro kwenda Mwanza.



# Pochi la Mama Samia lafunguka



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi Innocent Bashungwa, amesema 'Pochi la Mama' yaani Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, limefunguka ambapo ametoa Sh. bilioni 97.1 kwa Daraja la Jangwani.

Amesema fedha hizo ni sehemu ya fungu zilizotolewa na Rais Dk. Samia kufuatia kuharibiwa kwa miundombinu ya barabara na madaraja kulikosababishwa na mvua za El Nino mwishoni mwa mwaka jana na mapema mwaka huu.

Alisema hayo jijini Dar es Salaam jana katika hafla ya utiaji mkataba wa ujenzi wa daraja hilo unaotarajiwa kukamilika ndani ya miaka miwili.

Alisema ujenzi wa daraja hilo lenye urefu wa mita 390 litahusisha pia ujenzi wa barabara za maungio zenye urefu wa mita 700 kwa pande zote mbili za daraja.

"Tunakwenda kujenga daraja ambalo tutasahau kero ambazo wana Dar es Salaam walikuwa wakipata pale Jangwani kila mvua ikinyesha, barabara tunasimamisha kwa sababu ya kujaa kwa maji.

"Ujenzi wa daraja hili tunakwenda kusahau, tunamshukuru sana Rais Dk. Samia kwa kutuwezesha kufanya jambo hili ambalo wana Dar es Salaam tumekuwa tukilisubiri kwa miaka mingi," alisema.

Alisema anawashukuru pia wananchi wa Dar es Salaam kwa subira kwani hata mwaka jana walipotembelea eneo la Jangwani wakati wa mafuriko wananchi walisema kila mwaka wimbo wenu ni huo huo, lakini baada ya ziara ile waliwaambia kwamba Rais Dk. Samia si Rais wa maneno mengi bali ni wa vitendo zaidi.

"Tuliwaahidi kabla ya mvua za Desemba, mwaka huu, tutakuwa tumekwishakamilisha masuala ya usanifu na kumpata mkandarasi, sasa wana Dar es Salaam, mmeona wanasema mwenye macho haambiwi tazama, leo (jana) mmemwona mkandarasi yule pale amesaini mkataba wa ujenzi wa daraja hilo ili kazi ianze," alisema.

Alisema Wizara ya Ujenzi ina wajibu wa kujenga daraja hilo wakati ujenzi wa kingo za bonde la Mto Mzimbazi Tamisemi wapo mbioni kuanza kutekeleza mradi huu.

Alisema Sh. bilioni 125 zipo katika hatua ya mwisho sasa hivi kuanza ujenzi wa daraja hilo.



Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa

# Dk. Slaa awaumbua viongozi wa Chadema

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEWAHI kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Willibrod Slaa, amekosoa vikali viongozi wa sasa wa chama hicho kwa kushindwa kuwaongoza wananchi ipasavyo na kutokujenga uelewa wa kutosha juu ya wajibu wao wa kisiasa.

Akizungumza kupitia Jukwaa la Clubhouse mwishoni mwa wiki iliyopita, Dk. Slaa alisema Chadema imeshindwa kuwapatia wananchi ujasiri na uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa nchini, hali iliyosababisha wananchi kubaki katika hali ya kutojiamini na kutegemea zaidi uongozi wa chama kuliko kuwa na nguvu zao wenyewe.

Katika mazungumzo yake, Dk. Slaa alitilia mkazo umuhimu wa chama kuwa na mikakati ya kuwajengea uwezo wananchi, akieleza kuwa kwa muda mrefu wananchi hawajawahi kupewa mwongozo madhubuti wa kujitegemea katika harakati za kisiasa.

"Usitegemee wananchi wawe mstari wa mbele, wanahitaji kuongozwa... Chadema mliwajengea uwezo? Upi? Kama mliwajengea uwezo wamefika wakashindwa kutekeleza, wananchi wajibu wao ni nini," alihoji.

Alisema jukumu la viongozi wa kisiasa ni kuwaongoza wananchi na kuwapa moyo wa kusimama kidete kwa ajili ya haki zao.


Alitoa mfano wa matukio mbalimbali ya siku za hivi karibuni likiwamo la Baraza la Wanawake wa Chadema (Bawacha) kuchoma vitenge vilivyokuwa vimetolewa kama zawadi na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema tukio kama hilo ni ishara ya namna ya chama kimeshindwa kuleta ushawishi wa kutosha kwa wananchi.

"Kwenye suala hili kwa mfano la kuchoma vitenge, wananchi hawakumualika Rais Samia, ninyi viongozi ndiyo mlimwalika. Mlikwenda kama chama kusema ulitupa zawadi sasa leo tunataka kuchoma hizi zawadi na mkachoma mbele yake? Wananchi mtawaingiza kwenye matatizo tu bila sababu," alisema Dk. Slaa na kuongeza:

"Wananchi wana jukumu lao, wananchi mliwaomba kwenye maandamano wametokea. Wananchi wanahitaji kupewa ujasiri na kauli za vyama vya upinzani juu ya maandamano zilitokaje?"

Kuhusu maridhiano Dk. Slaa alisema hayakuwa shirikishi kwani Chadema walikaa kwenye meza moja na serikali katika mchakato wa maridhiano bila kuwa wazi kwa wananchi.



Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Dk. Willibrod Slaa.

# Mamia ya vijana wajadili kupata ardhi nchini kwao

ZAIDI ya vijana 500 kutoka mataifa mbalimbali ya Afrika, juzi Jumatatu, walikutana jijini Arusha kujadili namna watakavyopata fursa na haki ya kumiliki ardhi katika nchi zao na kuitumia kujikwamua kwenye umaskini.

Mkutano ulioandaliwa na Taasisi ya Kimataifa inayofuatilia haki za vijana katika masuala ya ardhi kwa ushirikiano na Umoja wa Afrika (AU) na Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), unalenga kuwakutanisha pamoja vijana na wadau wengine wakiwemo viongozi wa serikali na taasisi za kiraia, ili kujadili namna ya kuwawezesha vijana kufahamu umuhimu wa ardhi na namna ya kuitumia kujikwamua kimaisha.

Wakizungumza katika mkutano huo unaofanyika wakati ambao asilimia kubwa ya vijana wa nchi za Bara la Afrika wanategemea kupata ardhi kwa kurithi baada ya wazazi wao kufariki dunia, baadhi ya vijana walisema kuwa wakati umefika wa Serikali za Afrika kuweka sheria na sera rafiki zinazotekelezeka na zenye tija kwa vijana.

Mkutano huo pia ulileta pamoja wataalam wa ardhi kutoka serikali za baadhi ya nchi za Afrika ikiwemo Tanzania ambao walisema kwamba kuna haja kubwa ya kuongeza nguvu kuwawezesha vijana kuelewa umuhimu wa ardhi na namna inavyoweza kuwasaidia katika harakati za kukabiliana na hali ya umaskini.


BBC.






# Maoni ya Mhariri & Uchambuzi

## HII NI KERO



## Tulimieni hii barabara

Sisi wakazi wa Tanga tunatumia barabara ya kutoka Handeni hadi Kilindi tunataabika sana na ubovu wa barabara.

Tunashukuru kuona kuna juhudi za kutengeneza hii barabara kwani kuna maeneo wakandarasi wako kazini.

Hata hivyo eneo kubwa la barabara gari haiwezi hata kwenda kilometa 30 kwa saa isipokuwa maeneo ya mwishomwisho kama unatokea Handeni ambayo yamelimwa.

Tunaomba wakati wakandarasi wakiendelea na kazi barabara hii ilimwe ili kuturahisishia usafiri.




MAONI YA MHARIRI

# Tujitokeze kugombea nafasi serikali za mitaa

Mwanzoni mwa wiki hii Waziri Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa alitoa mwito kwa Watanzania wenye sifa kujitokeza kuchukua fomu ili kugombea nafasi za uongozi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji katika uchaguzi utakaofanyika nchini kote Novemba 27, 2024.

Waziri ametoa wito huo wakati akitoa taarifa kwa vyombo vya habari mkoani Dar es Salaam kuhusu mchakato wa uandikishaji wapigakura ulivyokwenda na kuweka wazi kwamba fomu kwa ajili ya kugombea nafasi hizo zitaanza kutolewa Jumamosi ijayo, Oktoba 26, 2024 hadi Novemba 1, 2024.

Waziri amevisisitiza vyama vya siasa kuhamasisha wanachama wao kujitokeza kwa wingi kusudi wananchi wawe na uwanja mpana wa kuchagua viongozi.

Tunaungana na Waziri kuwahimiza Watanzania wakiwemo vijana, wanawake na walemavu wanaoamini wana sifa wagombee nafasi hizi. Moja ya swali la kujiuliza kabla ya kuchukua fomu ni hili; Je, uko tayari kushughulikia changamoto za watu unaokwenda kuwaongoza kwa sababu utakuwa mzigo wako?

Na sisi wengine tuwashiwishi wale tunaoona kwamba wana uwezo wa kutuongoza wachukue fomu za kugombea. Tusiwashawishi kwa sababu tunakunywa nao pombe au kahawa au kwa sababu tunaswali nao kwenye nyumba za iibada au kwa kuwa tunategemea kunufaika binafsi na uongozi wao, la hasha. Bali ni kwa sababu kadri tunavyowafahamu kwamba wana uwezo wa kutuvusha kwenye safari ya maendeleo.

Kwa kuwa, kwa mujibu wa Katiba na sheria zetu, wagombea ni la lazima watokane na vyama, tunatarajia vyama pia vitatuletea wagombea mahiri, makini na ambao wana uwezo wa kuwatumikia wananchi.


Kwamba vyama vitapitisha wagombea waadilifu na waaminifu, wagombea wazalendo kwa nchi yao, wanaotanguliza maslahi ya nchi mbele na walio tayari kujitolea na kujitoa kwa ajili ya wananchi wenzao.

Tuepuka wagombea wenye mweleko wa kutumia rushwa ili kuwachagua kwani hao watatumia muda mwingi kurejesha gharama zao badala ya kututumikia. Wagombea wengine wa kuogopwa sana ni wale wenye mweleko wa kutugawa kwa aina yoyote ile.

Lakini tukumbuke pia sheria inatupa wananchi siku saba za kuweka pingamizi ambazo kuhusiana na sifa za mgombea, kutokubaliana na uteuzi wao, au sababu nyingine zinazoweza kuathiri haki ya mgombea kuwania nafasi husika.

## Wasiliana nasi

**Mhariri Mkuu:** +255713263775 / +255748115000
**Mhariri wa Habari:** +255768411003
**Mhariri Michezo:** +255784122020
**Meneja Masoko/Biashara:** + 255718480406 / + 255733768825
**S. L. P:** 15110, Dar es Salaam
**Makao Makuu Mtaa:** Barabara ya Morogoro
**Jengo la:** Aura Mall
**Chumba Cha Habari:** +255 (0)222151532
**Email:** uelekeohabari@gmail.com



Hamid Yassin
JICHO LANGU
0768 888 787

# Tuache chokochoko, tusubiri kampeni na uchaguzi

ZOEZI la uandikishaji wapigakura kwenye Uchaguzi ujao wa Serikali za Mitaa lilikwisha Jumapili iliyopita ya Oktoba 20 na limekwenda vema, ingawa kuna malalamiko ya hapa na pale.

Limekwenda vema kwa sababu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa amesema kuwa, jumla ya wapikura 26,769,995 sawa na asilimia 81 ya lengo la kuandikisha wapigakura 32,987,579, wameandikishwa kwenye Daftari la Wapigakura wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa hadi kufikia juzi.

Taifa huhitaji watu ili kupiga hatua, watu ndiyo wenye nchi, msingi wa nchi ni maamuzi ya wananchi kuchagua viongozi wao watakaoshiriki katika kuchagiza maendeleo.

Katiba yetu inatambua uwepo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Ibara ya 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977 inatambua uwepo wa Serikali za Mitaa.

Dhamira ya ibara ya 145 ni kusogeza mamlaka ya nchi kwa wananchi, viongozi wanaokusudiwa kuchaguliwa wanaotokana na wakazi wa eneo fulani ni msingi wa serikali kwa wananchi.

Ikumbukwe waliokuwa viongozi wa sasa wa Serikali za Mitaa kote nchini wameshamaliza muda wao tangu Oktoba 19, hivyo nafasi hizo lazima zipate wenyewe. Naam; kufikia lengo la kuandikisha wapigakura kwa asilimia 81 ni sehemu ya kutimiza vifungu hivyo hapo juu vya Katiba yetu, ili lengo litimie kwa asilimia 100, zimebaki hatua chache za kukamilisha zoezi hili zikiwemo zile za vyama kuchagua wagombea wao kwa taratibu zao.

Baada ya hapo utafuata utaratibu wa kuchukua fomu na kuzirejesha ambalo limepangwa kuwa kati ya Oktoba 26 hadi Novembva 1. Kitachofuata ni muda wa kampeni na hatimaye uchaguzi wenyewe Novemba 27, hivyo hapa hakuna tena muda wala nafasi ya kuleta blaablaa kwa vyama vyote vya siasa zaidi ya kuingia ulingoni.

> **Ikumbukwe waliokuwa viongozi wa sasa wa Serikali za Mitaa kote nchini wameshamaliza muda wao tangu Oktoba 19, hivyo nafasi hizo lazima zipate wenyewe. Naam; kufikia lengo la kuandikisha wapigakura kwa asilimia 81 ni sehemu ya kutimiza vifungu hivyo hapo juu vya Katiba yetu, ili lengo litimie kwa asilimia 100.**

Haya malalamiko ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kupitia Mwenyekiti wao wa Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema eti kwani Waziri Mchengerwa ametangaza mapema majina ya waliojiandikisha hayana mantiki kabisa kwa wakati huu.

Dhamana ya uchaguzi huu na nchi kwa ujumla hivi sasa ipo mikononi mwa vingozi wa vyama hivi vya siasa, hivyo si busara hata kidogo kuanzisha maneno ya chokochoko hivi sasa.

Kama nilivyosema, dhamana ya nchi iko mikononi mwenu viongozi, ushawishi wenu kuhusu amani katika kipindi hiki ndio utakaoliokoa taifa la Tanzania ama utaliingiza taifa katika vurugu na mfarakano.

# Je; ulaji wa mkate una athari za kiafya mwilini?




MKATE umekuwa chakula kikuu kwa zaidi ya miaka 10,000.

Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni, imekuwa ikielezwa kwamba husababisha shinikizo la damu na ugonjwa wa kisukari, wakati hali hizi sugu zimekuwa nyingi.

Ukweli ni kwamba matumizi ya aina fulani ya mkate huhusishwa na hatari ndogo ya ugonjwa wa moyo na mishipa.

Mkate ni chanzo cha wanga, nyuzinyuzi za lishe, vitamini na madini.

Nyuzinyuzi ni muhimu kwa usagaji chakula na kuzuia magonjwa kama saratani ya utumbo mpana na unene uliopitiliza.

Ulaji uliopendekezwa wa kila siku wa gramu 25 za nyuzi, unaweza kufanikishwa kwa kula mkate.

Kabohaidreti tata huwa na athari ya wastani na endelevu kwenye glukosi ya damu ambayo inaweza kusaidia kuzuia upinzani wa insulini na hatimaye aina ya pili ya kisukari.

Glucose ndiyo chanzo kikuu cha nishati mwilini.

Jambo kuu siyo uwepo wake katika chakula, lakini jinsi inavyoingizwa haraka ndani ya damu.

Fahirisi ya glycemic ya aina fulani za mkate ni ya chini ikilinganishwa na vyakula vingine vyenye sukari rahisi.

Kwa kuongeza, uwepo wa nyuzi hupunguza kasi ya ulainishaji (digestion) na ngozi ya glucose.

**JE, MKATE NI CHAKULA KILICHOSINDIKWA ZAIDI?**

Ulaji mwingi na wa mara kwa mara wa vyakula vilivyosindikwa na vyakula vilivyoongezwa sukari na mafuta (hasa vilivyo na asidi ya mafuta yaliyojaa) huchangia hatari ya magonjwa sugu.

Mkate, hata hivyo, si lazima uwe katika kategoria hii.

Kuingizwa kwa nafaka nzima katika uundaji wa mkate kunahusishwa na hatari iliyopunguzwa ya ugonjwa wa kisukari cha aina ya pili, fetma na ugonjwa wa moyo.

Ulaji wa nafaka zisizokobolewa, kama zile zinazopatikana katika mkate wa ngano, huhusishwa na kupunguza kwa kiasi kikubwa hatari ya vifo kutokana na ugonjwa wa moyo na mishipa na saratani.

**MKATE UNAWEZA KUWA SEHEMU YA LISHE YENYE AFYA**

Haya yote yanasisitiza umuhimu wa kuzingatia ubora wa mkate na ulaji wa afya badala ya kutoa taarifa za kina kuhusu hatari yake.

Mkate hauna madhara kwa asili. Madai makubwa kuhusu matumizi yake yanapuuza ugumu wake.

Kama sehemu ya lishe bora na vyakula vibichi, nafaka nzima, matunda, mboga mboga na mafuta yenye afya, mkate unaweza kuwa nyongeza ambayo hutoa nishati na virutubishi muhimu.

Kulaumu chakula kimoja kwa matatizo mengi ya kiafya, huelekeza umakini kutoka kwa sababu halisi za hatari, kama vile ulaji mwingi wa vyakula vilivyochakatwa kwa wingi na mtindo wa maisha wa kukaa tu.

Ulaji wa wastani wa mkate, kwa kweli, unaweza kusaidia kuwa na maoni yasiyopotoshwa ya ukweli katika mwili wenye afya na kuridhika kwa muda mrefu.

BBC.

**Ulaji wa nafaka zisizokobolewa, kama zile zinazopatikana katika mkate wa ngano, huhusishwa na kupunguza kwa kiasi kikubwa hatari ya vifo kutokana na ugonjwa wa moyo na mishipa na saratani.**



# Wanachama 16 wa upinzani mbaroni tuhuma za uhaini

**KAMPALA, Uganda**

MAHAKAMA ya Kijeshi nchini Uganda, imewatia hatiani siku ya Jumatatu wanachama 16 wa chama cha upinzani kwa kosa la uhaini na umiliki wa vilipuzi kinyume cha sheria.

Taarifa hiyo ni kulingana na Wakili wa upande wa utetezi, Shamim Malende, ambaye alisema kesi hiyo ilikuwa na shaka kutokana na jinsi ilivyosikilizwa na baadaye watuhumiwa kukubali makosa ambayo awali waliyakana.

Upande wa mashitaka umedai kuwa wanachama 16 wa Jukwaa la Umoja wa Kitaifa (NUP) pamoja na wengine ambao bado hawajakamatwa, walikutwa na vilipuzi kati ya Novemba, 2020 na Mei, 2021, wakati uchaguzi ulikuwa ukiendelea.

Waandishi wa habari hata hivyo, hawakuruhusiwa kuhudhuria kikao hicho.

Vijana hao 16 wamekaa gerezani kwa miaka minne na watafikishwa mahakamani leo kusomewa rasmi hukumu yao.

**Kauli za kiongozi mkuu wa upinzani**




Kiongozi wa upinzani Robert Kyagulanyi maarufu kama Bobi WinePicha: Hajarah.

Mwimbaji wa zamani na kiongozi wa upinzani Robert Kyagulanyi maarufu kama Bobi Wine, amedai kuwa watu hao walilazimishwa kukiri makosa yao na kuomba msamaha wa Rais.

"Chochote ambacho Serikali ya Museveni inafanya, siku moja wale wote walio chini yake akiwemo yeye mwenyewe watawajibishwa" alisema Bobi Wine kuliambia shirika la habari la AFP, akisisitiza kuwa washtakiwa "walilazimishwa na maafisa wa serikali kukubali makosa hayo".

Tangu mwaka 1986, Uganda imetawaliwa na Rais Yoweri Museveni. DW.

# Kundi la M23 lauteka mji wa Kalembe

**KINSHASA, DR Congo**

KUNDI la waasi la M23, limeuteka mji wa Kalembe ashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kupanua wigo wake katika eneo hilo, Afisa mmoja na Mbunge wa zamani walisema juzi Jumatatu.

Kundi la M23 linaloongozwa na Watutsi, limekuwa likiendesha uasi katika taifa la Afrika ya kati lililokumbwa na ghasia tangu mwaka 2022.

DRC na Umoja wa Mataifa (UN), zinaishutumu nchi jirani ya Rwanda kwa kuliunga mkono kundi hilo kwa wanajeshi wake na silaha.

Hata hivyo, Rwanda inakanusha hili, lakini inasema imechukua kinachojulikana kama hatua za kujihami.

Waasi walikuwa wamekaa kilomita 10 kutoka Kalembe kwa takriban miezi minane kabla ya kuuteka mji huo siku ya Jumapili asubuhi kutoka kwa wanajeshi wa DRC na Wazalendo muungano wa makundi yenye silaha yanayoiunga mkono serikali, Kabaki Alimasi, Afisa kutoka eneo la Walikale ambako Kalembe ipo aliiambia Reuters.

Jeshi la DRC halikujibu mara moja ombi la kutoa maoni.

VOA.

# Rais mstaafu jela miaka 20 kwa ufisadi

**LIMA, Peru**

RAIS wa zamani wa Peru, Alejandro Toledo (78), amehukumiwa kifungo cha miaka 20 na miezi sita jela kwa kosa la kula rushwa.

Hukumu hiyo ni kutokana na kashfa ya ufisadi inayoihusisha kampuni kubwa ya ujenzi ya Brazil, Odebrecht.

Mahakama katika Mji Mkuu wa Lima, imegundua kuwa Toledo, ambaye aliitawala Peru kuanzia mwaka 2001 hadi 2006, alikubali rushwa ya Dola milioni 35 ili kutoa kandarasi ya kujenga sehemu ya Barabara Kuu inayounganisha mji wa Brazil wa Rio de Janiero hadi Lima.

Kesi hiyo inachukuliwa kuwa kashfa kubwa zaidi ya ufisadi katika eneo la Amerika Kusini.

Peru ilitoa waranti wa kukamatwa kwa Toledo mwaka 2017 na kuomba uhamisho wake kutoka Marekani, ambako alikimbilia baada ya kuondoka ofisini.

Toledo amekuwa akikanusha madai hayo na kuyataja kuwa yamechochewa kisiasa. DW.




Rais wa zamani wa Peru, Alejandro Toledo (katikati).

# Wanne wauawa Lebanon shambulio la anga la Israel

**BEIRUT, Lebanon**

WATU wanne akiwemo mtoto, wameuawa katika shambulizi la anga la Israel karibu na Hospitali Kuu ya Serikali Kusini mwa Beirut, Wizara ya Afya ya Lebanon inasema.

Shambulizi hilo lilionekana kulenga maegesho ya magari ya Hospitali ya Chuo Kikuu cha Rafik Hariri, chanzo cha hospitali kililiambia Shirika la Habari la Reuters.

**Wizara ya Afya ilisema watu 24 wamejeruhiwa.**

Ilikuwa ni miongoni mwa mashambulizi 13 ya anga yaliyokumba Beirut Kusini Jumatatu jioni.

Jeshi la Israel lilisema lilikuwa linashambulia vituo vinavyohusishwa na Hezbollah.

Msemaji wa Israel hapo awali alikuwa amewaonya watu kuhama kutoka maeneo kadhaa kusini mwa Beirut, hata hivyo hospitali ya Rafik Hariri haikuwa miongoni mwa maeneo yaliyotajwa.

Video kutoka kitongoji cha Dahiyeh Kusini mwa Beirut, ambapo maeneo saba yatakayolengwa yalitangazwa mapema, zilionyesha wenyeji wakikimbia kwa magari na kwa miguu huku mashambulizi hayo yakianza.

Eneo moja lililotambuliwa kama shabaha ya Jeshi la Israel lilikuwa takriban mita 400 kutoka Uwanja wa Ndege wa Beirut, ambao ndiyo pekee wa kimataifa unaohudumia Lebanon.

Vyombo vya habari vya ndani vilishirikisha picha za baadhi ya madirisha katika jengo la uwanja wa ndege ambayo yalilipuliwa katika mlipuko huo.

Israel haijatoa maoni yoyote tangu ilipotoa maonyo ya awali ya kuwahamisha.

Awali, Jeshi la Israel lilikuwa limesema mapema Jumatatu kwamba liligundua ngome ya Hezbollah iliyojificha chini ya hospitali tofauti kusini mwa Beirut, ambayo tangu wakati huo imehamishwa.



Msemaji wa IDF Admiral Daniel Hagari alisema bila kutoa ushahidi kwamba chumba cha kulala chini ya hospitali ya Sahel huko Haret Hreik kilikuwa na mamia ya mamilioni ya dola taslim na dhahabu ambazo zilikuwa zikitumika kufadhili mashambulizi ya Hezbollah dhidi ya Israel.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa Hospitali ya Sahel alikanusha kuwa kulikuwa na chumba cha kulala chini yake na kutoa wito kwa Jeshi la Lebanon kukagua eneo hilo.

Israel inaonekana kupanua vita vyake dhidi ya Hezbollah zaidi ya miundombinu ya kijeshi na inasema inalenga mitandao ya kifedha ya kundi hilo.

Mkuu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi wa Kipalestina (Unrwa) alisema Israel inaendelea kuzuia misheni ya kibinadamu kufika kaskazini mwa Gaza ikiwa na vifaa muhimu kama chakula na dawa.

"Hospitali zimeshambuliwa na kuachwa zimelemazwa huku watu waliojeruhiwa wakiachwa bila huduma," Philippe Lazzarini aliandika kwenye mtandao wa X.

Pia alisema makazi yaliyosalia ya Unrwa yalikuwa yamejaa kupita kiasi hivi kwamba watu waliokimbia makazi wanalazimika kuishi kwenye vyoo na akataja ripoti kwamba watu wanaojaribu kukimbia walikuwa wakiuawa.

Jeshi la Israel limekuwa likizidisha mashambulizi ya wiki moja katika maeneo ya kaskazini mwa Gaza dhidi ya kile ilichosema ni wapiganaji wa Hamas waliojikita tena huko.

Siku ya Jumatatu wakazi na madaktari walisema vikosi vya Israel vilikuwa vinazingira hospitali na makazi ya watu waliokimbia makazi yao.

Jeshi la Israel lilisema linarahisisha uhamishaji wa raia na kuhakikisha hospitali zinaendelea kufanya kazi huku likiendelea kukabiliana na magaidi na miundombinu ya kigaidi.

BBC.

*Leo yetu ndiyo kesho yetu*

Uelekeo

JARIDA

# Jungu kuu

| Jumatano Oktoba 23 - 29, 2024 |

UTALII AFYA JAMII

Jarida hili haliuzwi



# Tusichague viongozi alimradi, tusimame kwenye vigezo hivi:

UK. 12 & 13




# Kwa jinsi hii, bado CCM itashinda kwa kishindo

**Na Shaphy Pinda, Newala**

Uchaguzi ni nguzo ya kupima kiwango cha demokrasia kwani ni kitu kinachowapa fursa wananchi uhuru wa kuchagua na kuchaguliwa.

Kwa lugha nyingine, demokrasia ni mfumo wa serikali ambao mamlaka ya uongozi yanayotokana na ridhaa ya wananchi husika na kila mtu anakuwa na haki ya kushiriki kwenye serikali hiyo moja kwa moja au kupitia uwakilishi wa wajumbe aliyowachagua.

Ibara ya 5-(1) ya Katiba inabainisha kwamba "kila raia wa Tanzania aliyetimiza umri wa miaka 18 anayo haki ya kupiga kura katika uchaguzi unaofanywa Tanzania na wananchi."

Watu wanapaswa kutambua kwamba; "uchaguzi ni njia inayowapa wananchi hiari ya kushiriki kuweka mamlaka itakayosikiliza matakwa yao na kuyatendea kazi kwa maendeleo yao".

Sanjari na hilo, haki na uhuru wa watu kuweka mamlaka waitakayo kupitia wawakilishi wawatakao kwenye serikali ndiyo msingi wa utawala wa kidemokrasia. Kwa hiyo basi, msingi huu unazingatia uchaguzi wa vipindi, uchaguzi bora (huru na haki), haki ya kugombea, haki ya anayestahili kuchagua, usawa katika kupiga kura, kura ya siri na matakwa ya wapiga kura kuheshimiwa haki zao.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazojitahidi kuheshimu mfumo wa kidemokrasia ambapo inatoa uhuru wa vyama vya siasa kushiriki katika uchaguzi ambao unafanyika kila baada ya miaka mitano kwa uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

Mwaka huu tuna uchaguzi wa serikali za mtaa utakaofuatiwa na uchaguzi mkuu mwaka kesho na bila shaka wengi wetu na wewe unayesoma hapa umejiandikisha kwenye Orodha ya Mpiga kura mtaani kwako.

Tukija kwenye suala la kushinda uchaguzi si jambo ambalo linatokea tu bali ni jambo linalohitaji mipango madhubuti kufanikisha ushindi.

Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni chama kikongwe ambacho kimetokana na muunganiko wa Tanganyika African National Union (TANU) na Afro Shirazi Party (ASP). Kutokana na ukongwe wake umekijengea uzoefu na uimara kwenye kushinda uchaguzi kutokana na sera na falsafa nzuri.

Ni matumaini ya chama chochote cha siasa kushinda uchaguzi, CCM inatanabaisha hili kwenye malengo na madhumuni yake kwenye ibara ya 5-(1) ya katiba ya CCM, toleo la Desemba 2022 linalosema kwamba "CCM ina lengo la kushinda katika uchaguzi wa serikali kuu na serikali za mitaa Tanzania Bara na Zanzibar ili kuunda na kushika serikali zote mbili..."

Kutokana na hili, mwaka 2021 kwenye Mkutano Mkuu Maalumu wa CCM Taifa ambao ulimchagua Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kura 1862 kuwa mwenyekiti wake, aliwakumbusha wana CCM kwamba ushindi wa uchaguzi utaletwa kwa namna serikali itatekeleza ilani ya uchaguzi.

Vilevile, Dk. Samia alisema; "Nachukua jukumu hili la kukiongoza chama hiki nikiwa natambua kwamba kina changamoto nyingi hususani vyombo vya usafiri vya kutendea kazi, kwa mfano baadhi ya mikoa na wilaya hawana vyombo vya usafiri vya kutendea kazi kiasi kwamba jambo hili linadumaza na kufifisha shughuli za chama na kushindwa kufikia malengo yake kwa urahisi. Nataka nitumie fursa hii kuwaahidi kuwa tutashirikiana na nyinyi kuzitatua na kuzipatia ufumbuzi ili chama kiende mbeli".

Usafiri ndani ya vyama vya siasa ni nyenzo muhimu sana kwenye kuwafikia wananchi na kukifanya chama kitambulike na kionekane nini kinafanya. Ahadi hii kwa kiasi kikubwa imetekelezwa vyema kuanzia ngazi ya mkoa na wilaya wakipata magari mapya na sasa ngazi ya kata wamepatiwa vyombo vya usafiri (pikipiki) kwa watendaji wote wane, yaani katibu wa chama kata na makatibu wa jumuiya za chama watatu.

Kwa hiyo vyama vinavyopambana na CCM vijue hiki chama kina vitu vingi vya kukiwezesha kushinda uchaguzi kwa kishindo na kinachotakiwa ni kuendelea kujifunza kutokana nacho.

Katibu wa CCM Wilaya ya Newala, Robert Mwega akiongea kwenye kikao cha mafunzo ya udereva wa pikipiki za makatibu kata wa CCM na jumuiya zake alisema: "Leo mmekamilisha mafunzo ya pikipiki yatakayowawezesha kutumia vyombo hivi, ni matumaini yangu vyombo hivi vitakuwa msaada wa chama na si vinginevyo. Lengo letu ni ushindi wa mitaa, vijiji na vitongoji vyote, hivyo naomba mkawafikie wanachama kwenye matawi yote na mashina yote ili watambue jukumu lililoko mbele yetu."

Kadhalika, ushindi wa chama upo kwenye kuchagua viongozi wanaokubalika na wenye sifa za uongozi ambao wanazingatia sifa na miiko ya uongozi ndani ya Chama.

Mwalimu Nyerere aliwahi kusema "Chagueni mgombea ambae atakwenda kukidhi matakwa ya wananchi siyo matakwa yenu wapiga kura..." Hili CCM wamekuwa wakilizungatia sana kwani wanajua mgombea atakayechaguliwa haendi kuwaongoza wana CCM pekee bali watu wote bila kujali itikadi za vyama vyao.

Hivyo, pamoja na uzoefu, msisitizo ni kwamba Chama Cha Mapinduzi ni lazima kiwekee mkazo kwenye kuteua wagombea wenye siha njema, wenye maadili, wagombea wenye sifa ya kuheshimu watu, wanaopenda watu na kuwatumikia ipasavyo.

Sambamba na hilo, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi, Ally Salum Hapi alipokuwa kwenye ziara yake mkoani Pwani alisema; "Chama chetu kina utaratibu mzuri sana katika uchaguzi. Muda unapofika na kila muda wa uchaguzi tunasisitiza suala la kupata wagombea bora tutakaowauza kwa urahisi ambao wanakubalika na wananchi na siyo anayekubalika kwenye mifuko ya watu wachache. Kiongozi ambaye anazijua shida za wananchi na uchaguzi wa ngazi za mitaa ndio msingi wa uchaguzi mkuu."

Suala la ubora wa wagombea halipingiki kwani ubora wa viongozi ndio chachu ya ushindi wa chama chochote ulimwenguni na tukubali tusikubali Chama Cha Mapinduzi kimekuwa tanuri la kupika viongozi wenye sifa na vigezo vya kutumikia wananchi.

Hivi karibuni, Mchungaji Peter Msigwa aliyejiengua Chadema na kutimkia CCM alionesha wasiwasi kama chama hicho alimokuwa kinaweza leo kikawa na safu ya kutosha ya viongozi sahihi endapo kitapewa nchi kuanzia Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri hadi viomozi wa ngazi za chini!

Kuna kauli zinasema "umoja ni nguvu" na "umoja ni ushindi" hizi zote zinaonyesha ili jamii yoyote iweze kuwa na nguvu ni lazima iwe na umoja na kwenye umoja ni rahisi kushinda, Chama Cha Mapinduzi kinapoelekea kwenye chaguzi hizi kinasisitiza suala la mshikamano kama ambavyo imefafanuliwa vyema kwenye katiba ya CCM toleo la Desemba 2022, ibara ya 15-(1).

Ibara hiyo inasema; "Kila mwanachama anapaswa kutambua kwamba CCM ndicho chama chenye nguvu, uwezo na kwamba nguvu hizo zinatikana na umoja wa wanachama..."

Haipingiki kwamba CCM ina idada kubwa ya wanachama, kitu kinachopelekea kuwa na mtaji mkubwa wa watu wa kukiwezesha kushinda uchaguzi, hivyo basi juhudi katika kuelekea uchaguzi zinawekezwa kwenye kuandikisha wanachama wao kwenye daftari la kupiga kura na haya yalisisitizwa Makamu mwenyekiti wa CCM taifa kwa upande wa Zanzibar ndugu Dk. Hussein Mwinyi wakati anaongea na kamati za siasa za ngazi zote kuanzia matawi mpaka mkoa alipokua Pemba.

Dk. Mwinyi alibainisha; "Nimependa kukutana na kamati za ziasa za ngazi zote kuanzia matawi mpaka mkoani kwa maana kamati za siasa ndizo kamati za mkakati madhubuti kufanikisha ushindi, hivyo basi nasisitiza ya kwamba kujitokeza kujiandikisha kwenye daftari la kupiga kura ndio msingi wa kwanza kipindi hiki kwa maana tunaweza tukawa hamasa zote, shangwe zote na mipango ya kila aina lakini kama hatupo kwenye daftari la kupiga kura hatuwezi kushinda uchaguzi, naomba nitoe rahi ya kuwa viongozi tuende mpaka kwenye mashina tuwasisitize wanachama wetu wajiandikishe kisha kipindi cha uchaguzi wajitokeze kupiga kura na safari hii wale wenzetu wanaopanda kulalamika safari hii tuwaache mbali mpaka washindwe kulalamika".

Kwa mikakati hii ya kuhimiza wanachama wao kuanzia mashina kwa hakika ushindi ni mipango na CCM imejipanga kushinda.

Nikiwa natamatisha makala hii, napenda kusema kwamba ukipanga kushinda ni rahisi kushinda kwani ushindi wowote hauji tu bali unategemea mipango na dhamira ya dhati ya kufanikisha ushindi na kwa muundo wa Chama Cha Mapinduzi kuanzia kwenye mashina ambako ndiko wananchi wanakopatikana wananchi kwa mkazo huu hakika chama kinakwenda kushinda na ndio maana pale wanaposema kwenye ule wimbo "waache waisome naomba eehh, CCM mbele kwa mbele" ni kweli wanamaanisha.

Upinzani kazi yao itakuwa kusoma namna tu maana kwa mipango madhubuti kufanikisha ushindi kwao ni jambo linalowezekana.

*Mwandishi wa makala haya ni Mwalimu kwa Taaluma, Halmashauti ya Mji Newala mkoani Mtwara. Anapatikana kwa namba: 0620339559. Barua pepe: ashafii2050@gmail.com.*

# Uzalendo, uadilifu na umoja ni nguzo za taifa

**Na Hamid Yassin**

WIKI iliyopita, Oktoba 14 Tanzania ilihitimisha kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru ambapo Rais wetu, Dk. Samia Suluhu Hassan alihimiza uzalendo na uadilifu katika utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na serikali na wadau wengine wa maendeleo.

"Tumehitimisha kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru pamoja na Wiki ya Vijana hapa mkoani Mwanza. Ninawashukuru wote waliojitokeza kushiriki tukio hili la kihistoria ambapo Mbio za Mwenge wa Uhuru zimefikisha miaka 60. Pongezi kwa wote walioshiriki kuukimbiza kwa mwaka huu na kazi nzuri waliyofanya ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo," aliongea Dk. Samia.

Akaendelea kusema: "Nimepokea taarifa ya miradi yote iliyotembelewa katika mbio hizi ambayo inakwenda kunufaisha wananchi kwenye kila kona ya nchi yetu. Nimepokea mapendekezo na salamu za wananchi wa maeneo yote ulikopita Mwenge wa Uhuru, na kwa umakini na uharaka tutayafanyia kazi yale yote yaliyoainishwa kwa manufaa ya Taifa letu."

Dk. Samia, mbali ya siku hiyo kuzindua kitabu cha 'Historia na Falsafa ya Mwenge wa Uhuru', pia aliweka wazi kuwa, kupitia Mbio hizo za Mwenge wa Uhuru nchi nzima, ndiko madudu mengi yanayofanywa na watu waliokabidhiwa dhamana ya kusimamia miradi ya taifa, hubainika.

Baadaye siku hiyo, Dk. Samia akaagiza Mwenge huo wa Uhuru upelekwe kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro ili kuitangazia dunia kuwa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ni imara na pia utaendelea kulinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Naam; kupandishwa kwa Mwenge wa Uhuru Mlima Kilimanjaro, Paa la Afrika, mwaka huu 2024 kunaleta hamasa ya uzalendo kwa wananchi hususan wakati huu ambao Tanzania inaadhimisha miaka 60 ya uhuru na mafanikio ya taifa.

Jumamosi Oktoba 19 askari waliokabidhiwa kufikisha Mwenge na Bendera ya Taifa kwenye paa la Afrika, walifanikiwa kutekeleza kazi hiyo adhimu na askari walionekana ni wenye furaha kukamilisha kazi hiyo.

Tanzania inapopambana kukuza uchumi wake hususani ule wa viwanda, inahitaji watendaji na wananchi wazalendo, waadilifu na wenye moyo wa utaifa ili kufanikisha azma hiyo.

Maneno haya wazalendo na waadilifu ni vyema niyafafanue kidogo.

Uadilifu kwa kifupi ni kufanya mambo sahihi na mazuri wakati wote, yaani mambo yanayokubalika na jamii na yasiyokiuka sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Maadili ni mambo mema wakati wote na hakuna maadili mabaya.

Uzalendo ni hali ya kuwa na mapenzi ya nchi na kiasi cha kuwa tayari kufa kwa nchi yako na pia kutanguliza mbele maslahi ya nchi na ya Watanzania kabla ya maslahi yako binafsi.

Kwa lugha nyingine, uzalendo ni kitendo cha mtu kuipenda nchi yake kwa moyo wa dhati, kutumikia taifa kwa manufaa ya wote, kujali, kulinda na kuthamini rasilimali zilizomo na kuhakikisha zinanufaisha Watanzania wote.

Uzalendo katika nchi ndio chanzo cha maendeleo na usawa kwa watu wote, uzalendo unaleta haki, unajenga misingi ya kuthamini, kujali binadamu wenzio, uzalendo ndio chachu ya kulinda, kutunza na kuzitumia rasilimali kwa manufaa ya Taifa.

Baba wa Taifa, hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere mara baada ya Uhuru alikuja na mwongozo wa 'Imani na Ahadi za TANU (chama kilichokomboa nchi cha Tanganyika African National Union).

Ahadi hizi zilikuwa msingi mkubwa wa kujenga uzalendo wa nchi hii, ambapo mpaka sasa imani na ahadi hizo bado zina mantiki katika kuimarisha Taifa kuelekea uchumi wa viwanda.

"Binadamu wote ni sawa na ni ndugu zangu. Nitaitumikia nchi yangu kwa faida ya wote, rushwa ni adui wa haki sitatoa wala kupokea rushwa, nitajitolea nafsi yangu kuondoa umasikini, ujinga, magonjwa na dhuluma".

Aidha, yote hayo Mwalimu alifanya kwa masilahi mapana ya Tanzania akijua wazi katika misingi hiyo ya 'Imani na Ahadi za TANU' ilikuwa ni sehemu ya kuweka uadilifu na utumishi uliotukuka kama mtumishi wa umma.

Pia, kama Mtanzania ambaye yupo katika jamii kwa namna moja au nyingine kujumuika kwa pamoja kuleta maendeleo kuelekea uchumi wa kati na viwanda tunaoulilia siku zote.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dk. Samia ambaye ni mzalendo namba moja kwa sasa, binafsi kwa vipimo vyovyote vile, mchango wake ni mkubwa mno. Falsafa ya Mwenge ambao ameagiza ufike tena Mlima Kilimanjaro, mbali na ujumbe wake na kukagua miradi inabeba uzalendo, kuimarisha misingi ya amani, umoja, upendo, mshikamano. Mwenge pia unahamasisha shughuli za maendeleo katika jamii yetu na kupelekea kwa Watanzania wote ujumbe maalumu uliokusudiwa na Serikali kila mwaka.

Kaulimbiu ya Mwenge wa Uhuru kwa mwaka 2024 ilikuwa ni "Tunza Mazingira, Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ujenzi wa Taifa Endelevu."

Ikumbuke kwamba kaulimbiu wakati Mwenge unawashwa mwaka 1961 na ambayo imekuwepo wakati wote ni kumulika ndani na nje ya mipaka yetu ili kuleta matumaini na upendo badala ya chuki miongoni mwetu.

Haitoshi viongozi wetu kuwa wazalendo peke yao bila sisi wananchi pia tuna dhima ya kuhakikisha tunakuwa sehemu ya uzalendo ili kujenga uchumi wa viwanda katika nchi yetu.

Lazima tutafakari kwa makini na kujiuliza kila mmoja wetu mchango wake katika kuhakikisha sekta binafsi na baadhi ya taasisi zetu ziweze kuchangia kwa sehemu kubwa ufanisi wa uchumi wa viwanda.

Uzalendo unajenga undugu na kuleta amani, uzalendo hudumisha upendo, uzalendo unaleta ushirikiano. Hayo yote ni muhimu katika kufanikisha uchumi wa viwanda maana Waswahili husema; "Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu".

Pia, uzalendo unajenga misingi ya uwajibikaji kwa kila mmoja na kulitumikia taifa kwa moyo wote, uzalendo huondoa unyonyaji na matabaka ya kubaguana katika jamii.

Taifa lolote ambalo halina matabaka watu wanakuwa na imani ya kujituma kwa kuwa kinachopatikana ni chetu wote.

Uzalendo ni upendo na dhana ya hiari ya mtu binafsi, uzalendo hujengwa kutoka moyoni pia, hujengwa na wanajamii kupitia misingi ya maisha wanayoyaishi na itikadi ya kisiasa miongoni mwa wanajamii.

Hivyo mtu anaweza kuzaliwa na wazazi ambao ni wazalendo na kuendelea kujengwa katika misingi ya uadilifu ambapo jamii inayomzunguka ni ya kizalendo atabaki hivyo na kuonesha uzalendo maisha yake yote.

Nadhani, mtakubaliana nami kuwa Watanzania walio wengi ambao ni vijana takriban asilimia 60 ya Idadi ya watu Tanzania, sio wale waliolelewa na kujengwa na waasisi wa Taifa letu kwenye misingi ya uzalendo, umoja na mshikamano.

Sio sahihi kwa wale wanaodhani dhana ya uzalendo ni simulizi ya kufikirika au itikadi iliyopitwa na wakati inayowanyima uhuru au inayovunja haki za binadamu.

La hasha, uzalendo ni mfumo wa maisha na mwelekeo ambao unamfanya mtu yeyote aone thamani ya nchi yake, fahari ya kuwa sehemu ya nchi yake, kujivunia umoja, ushirikiano, upendo, undugu na maelewano ya watu wa taifa lake.

Uzalendo huwakusanya watu wa Taifa husika kuwa na mtazamo mmoja mfano hai ni Tanzania ya viwanda yenye masilahi kwa Watanzania wote bila kubagua sura, rangi kabila na mambo kama hayo.

Dhana hii ya uzalendo inatakiwa kubebwa na Watanzania wote wapenda maendeleo, tusikubali kama Taifa kupoteza dhana hiyo na kila mtu kuwa na mwelekeo wake.

Hii itasababisha nchi kupoteza mwelekeo na hapo ndipo tutakapotoa mwanya kwa maadui zetu kutukwamisha kusudio letu la kuelekea uchumi wa kati na kuleta maendeleo.

Uzalendo huondoa matabaka katika jamii, unapokosekana, matabaka yanazidi kuongezeka na makundi ya kupoteza uzalendo wetu yanaongezeka kila siku.

Matokeo yake rasilimali za nchi zilizopo zinawanufaisha watu wachache na kuwaacha wenye nchi kutaabika na kudokoa macho bila kujua la kufanya.

Rais wetu mpendwa, Dk. Samia amekuwa akiliona hilo na kulishikia bango kwa kuwa anajua likiachiwa liendelee, mambo yataharibika kwa kiasi kikubwa na ndio maana amekuwa mstari wa mbele kujenga uzalendo na mshikamano na hata Falsafa yake ya R4 imejikita katika kujenga uzalendo kwa nchi yetu.

Taifa linahitaji jitihada za kila mmoja wetu kuhakikisha kuwa tunautetea na kuuendeleza uzalendo wetu kwa maendeleo yetu.

Ipo kila sababu ya kuunga mkono jitihada za Rais Dk. Samia ili kuhakikisha uzalendo unarejea nyumbani kwao ambapo sio pengine ila ni Tanzania.

Hakuna shaka kwamba, Mwenge wa Uhuru ni chombo pekee cha kitaifa kinachowaunganisha Watanzania na kuwa wamoja, kwani haufungamani na itikadi za kisiasa, ukabila wala udini. Mwenge wa Uhuru ni mali ya Watanzania wote.

*Kwa maoni na ushauri;*
*0768 888 787 ama 0784 122 020.*



# Tusichague viongozi alimradi, tusimame kwenye vigezo hivi:

**Na Hamisi Kibari**



NOVEMBA 27, si mbali sana, siku ambayo Watanzania tunatakiwa kwenda kuchagua viongozi muhimu sana kwenye vijiji vyetu, mitaa yetu na vitongoji vyetu.

Baada ya zoezi la kuandikisha wapiga kura kwenye orodha ya wakazi kumalizika, Jumatatu ya wiki hii, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mohamed Mchengerwa alitoa mwito kwa wenye sifa wajitokeze kuchukua fomu ili kugombea nafasi hizo za uongozi.

Mchengerwa alisema fomu kwa ajili ya kugombea nafasi hizo zitaanza kutolewa Jumamosi hii ya Oktoba 26, 2024 hadi Novemba 1, 2024.

Waziri alivihimiza vyama vya siasa kuhamasisha wanachama wao kujitokeza kwa wingi kusudi wananchi wawe na uwanja mpana wa kuchagua viongozi.

**UMUHIMU WA VIONGOZI HAWA**

Umuhimu wa viongozi wa serikali za mitaa katika jamii ni kutokana na kushughulikia masuala ya karibu na wananchi. Baadhi ya majukumu yao ni kuwa wawakilishi wetu kwa maana kwamba viongozi hawa ni kiungo kati yetu na serikali kuu, wakihakikisha matatizo na mahitaji ya watu yanawasilishwa kwa ngazi za juu.

Pia ndio wasimamizi wa rasilimali za vijiji na mitaa yetu kama ardhi, maji, na miradi ya maendeleo wakihakikisha raslimali zinatumika kwa manufaa ya wote. Lakini pia wana jukumu la kulinda na kusimamia usalama wa maeneo yetu kwa kushirikiana na sisi na vyombo vya dola. Pia wanahusika katika suala la kupatanisha migogoro na kuzuia uvunjifu wa amani.

Jukumu lingine la viongozi tunaokwenda kuwachagua ni utekelezaji wa sera na sheria kwa kuhakikisha wananchi wanatii taratibu za kisheria na kuhamasisha maendeleo katika maeneo yetu.

Kwa hiyo utaona viongozi hawa wanachangia kwa karibu sana maendeleo yetu na hivyo baada ya kujiandikisha hakikisha unashiriki kupiga kura. Usisibiri watu wakuchagulie kiongozi usiyemtaka. Chagua mwenyewe.

Makala hii inalenga kuangalia vigezo vya aina ya viongozi tunaowataka ambao tutawakabidhi jukumu la kuongoza mitaa, vijiji na vitongoji vyetu. Hawa ni watu ambao tunaishi nao mitaani na wengine tumekua nao pamoja na hivyo tunawafahamu vyema.

Lakini pia makala haya ni kioo cha wale wanaotaka uongozi kujipima kama wana sifa hizi. Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alipata kusema kwamba uongozi ni mzigo. Mtu mwaminifu na mwadilifu kabisa kabisa haukumbilii. Kwa nini? Akatoa majibu kwamba kwa sababu changamoto za watu unaowaongoza, ni mzigo wako.

Kwa sisi tunaoamini Mungu, pia misahafu inafundisha kwamba kila mchunga (kiongozi) ataulizwa kwa alichokichunga. Je, alifanya uadilifu?

**UAMINIFU NA UADILIFU**

Sifa ya kwanza kwa yeyote anayetaka uongozi anatakiwa kuwa mwaminifu na mwadilifu. Tukisema mtu mwenye maadili inaamisha mtu ambaye ana sifa za kufanya mambo sahihi, yanayokubalika na jamiii, kanuni na sheria bila kujali kama mtu anamuona ama hamwoni.

Kwa sababu hawa tunaokwenda kuwachagua ni wasimamizi wa raslimali zetu, basi wanapswa wawe na uwezo wa kutunza raslimali za umma kwa kuhakikisha zinatumika kwa kuhudumia umma na si kwa familia zao.

Kuhakikisha wanasimamia fedha za umma na si kutengeneza mipango ili kujinufaisha na fedha za miradi.

Katika kipengele hiki cha uadilifu na uaminifu ni pamoja na kuchagua wagombea wanaosema kweli tupu. Mtu asiye mkweli, mwenye kauli tata pia hatufai.

Pia tunategemea kiongozi anayeheshimu watu, wakubwa kwa wadogo sambamba na kuheshimu kazi tunayokwenda kumpa kwa maana kwamba awe tayari kuwatumikia watu na siyo kudhani watu watamtumikia yeye!

Ingawa wenyeviti wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji hawakutajwa kwenye Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Na. 13 ya mwa 1995, hususani Kifungu 6 (1), lakini wanapswa kufanya kazi kwa mujibu wa sheria zilizopo ikwemo hiyo ya maadili.

Kifungu hicho kinaeleza juu ya wajibu wa viongozi wa umma kudumisha uadilifu, kwa kuepuka migongano ya maslahi binafsi na ya umma. Kinawaelekeza kutanguliza maslahi ya umma mbele na kujiepusha na vitendo vinavyoweza kuathiri hadhi yao au taasisi wanazoziongoza (Kijiji, mtaa au kitongoji). Viongozi wa umma wanatakiwa kuwa waaminifu, wenye uadilifu, na kuheshimu sheria.

Kwa ujumla sheria hii inalenga kuhakikisha kuwa viongozi wanatenda haki na bila kutumia nafasi zao vibaya kwa manufaa binafsi.

## MGOMBEA NA RUSHWA

Katika kipengele hiki cha uaminifu na uadilifu pia kunaingia suala la rushwa.

Tafsiri mojawapo ya rushwa ni mtu kununua haki asiyostahili. Kwamba anatoa mlungula ili apewe upendeleo fulani.

Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere alipata kuonya vikali mtu anayewania uongozi kwa kutoa rushwa kwani swali la msingi la kujiuliza ni huyu mtu atazirejeshaje hizi fedha zake!

Kutokana na tatizo la rushwa katika jamii yetu, Mwalimu Nyerere pia alitutaka tuchague viongozi wanaochukia rushwa kwa dhati. Na kwamba anaposema ninachukia rushwa isiwe mdomoni tu bali tukimwangalia vizuri tuone hiyo inatoka moyoni kabisa kabisa.

Kwa lugha nyingine yeyote anayetoa rushwa katika uchaguzi ana lengo la kunufaika binafsi na nafasi hiyo na hivyo hatufai hata kidogo.

Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 ipo kudhibiti na kusimamia matumizi ya fedha wakati wa kampeni za uchaguzi, kuhakikisha uwazi na haki katika mchakato wa uchaguzi vinasimama.

Kwa hiyo yeyote anayevunja sheria kwa kugawa hata chakula, kununulia watu kadi hata kuwasafirisha, licha tu ya kuvunja sheria lakini huyo ni mtu wa kuepukwa sana. Lazima Watanzania katika uchaguzi huu wa Serikali za Mitaa na ule uchaguzi mkuu ujao mwakani tuhakikishe hatununuliki kijinga kiasi hiki!

Dhana ya kusema kipindi cha uchaguzi ni kipindi cha kuvuna kwa sisi wapiga kura ni dhana ya hovyo na hatari sana. Ni dhana inayosababisha kupeleka watu kwenye ofisi za umma kwenda kuzitumia vibaya kwa kutafuta maendeleo yao na familia zao badala ya maendeleo ya umma.

Kuchagua mtu kwa sababu amekuhonga chochote maana yake ni kuchagua mtu ambaye badala ya kutatua matatizo katika jamii yako yeye ndiye anachangia kuyaendeleza!

Mwanamajumui ambaye pia ni mwanaharakati, Profesa Patrick Loch Lumumba kutoka Kenya, katika hotuba zake amepata akiwashangaa wapiga kura wengi wa Afrika kupenda kuhongwa na wagombea uongozi.

Katika hilo anasema kinachotokea ni sawa na kununua pikipiki halafu wapiga kura wakategemea ifanye kazi kama Fuso!

Profesa akafananisha kipindi cha uchaguzi na hundi mpya (blank cheque) ambayo tunapewa ili tujaze fedha tunazotaka lakini tunazugika na rushwa kujaza fedha zisizotufikisha kokote!

Na kimsingi hasa, mgombea uongozi ni mtumishi wetu, ni mwakilishi wetu ni mtu anayetufanyia kazi sisi na hivyo ilitakiwa hasa sisi ndio tumgharimie mambo ya kampeni na si yeye.

Kwa hiyo dhana ya uadilifu ni msingi wa uongozi bora katika jamii yoyote ile, ambapo kiongozi anapaswa kutenda haki kwa watu wote, masikini na matajiri na bila kujali itikadi zao za vyama au dini. Kiongozi asiye mwadilifu na mwaminifu hawezi kusimamia haki kwa kila mtu na bila upendeleo.

Na katika kipengele cha uaminifu kinahusisha pia mtu kutekeleza majukumu kwa uangalifu na kuhakikisha mali ya umma haitumiwi vibaya.




## UWAJIBIKAJI

Sifa nyingine ya kiongozi Bora ni anayejali kazi yake. Kwamba ni mtu anayesimama kwenye wajibu wake na hivyo hata anaotuongoza tutawakibika kusimama kwenye nafasi zetu.

Kimsingi, ili aweze kusimamia wengine lazima na yeye awe mfano bora ili anaowasimamia wasipate nafasi ya kusema; "mbona yeye mwenyewe hafanyi, mbona yeye mwenyewe yuko hivi, yuko vile."

Tuchague viongozi ambao wako tayari hata kujiuzulu kwa makosa ya walio chini yao ili kulinda hadhi ya ofisi ya umma.

Katika eneo hili la uwajibikaji tuchague watu wasiosubiri majukumu yao yaje kufanywa na wakuu wa wilaya au wakurugenzi wa halmashauri husika.

Wawe viongozi wanaosimamia na uwajibikaji wa pamoja kwa maana kwamba lile linalopitishwa kwenye vikao, hata kama si msimamo wao, ndilo wanalopaswa kulisimamia.

Tuepuka sana viongozi wanaopenda kutumia maneno; "haya ni maagizo kutoka juu." Kutoka juu wapi?

## UZALENDO

Kigezo kingine cha kumfahamu kiongozi anayetufaa ni kuangalia uzalendo wake. Uzalendo ni hali ya mtu kuipenda, kuitetea na kuilinda nchi yake kwa uaminifu kiasi kwamba yuko tayari hata kufa kwa ajili ya nchi yake.

Ni mtu anayetanguliza maslahi ya Taifa kwanza kabla ya maslahi yake binafsi na familia yake. Ni mtu ambaye hata yuko tayari kutumia pesa zake za mfukoni ili kutekeleza jambo lenye maslahi kwa nchi au umma wa Watanzania.

Mara nyingi wanasema wenye kusema kwamba moja ya alama inayoonesha uzalendo wa mtu ni hali ya mtu kupenda kujitolea. Yaani mtu anayejali kufanya kazi kwa ajili ya umma bila kutanguliza kulipwa ujira au maslahi binafsi.

Kwa hiyo, kila mgombea aliyetia nia ya kutaka uongozi tumwangalie ni kwa kiasi gani yuko tayari kutoa raslimali zake binafsi, muda na nguvu zake kwa maslahi ya watu wengine?

Na hii iwe ni tabia yake ni si katika kipindi kama hiki cha kuelekea chaguzi. Kwamba kipindi ndipo tunaona anatoa misaada huku na kule lakini huko nyuma hatukumwona.

## UCHA MUNGU

Ingawa ni kweli kwamba kuna watu wanashinda misikitini na makanisani lakini wana tabia mbaya katika jamii, lakini aghalabu wacha Mungu wengi ni waadilifu pia.

Hii ni kwa sababu vitabu vitakatifu takribani vyote vinafundisha kutenda yaliyo mema na kukataza kufanya yaliyo mabaya (dhambi).

Kiongozi wa umma mwenye hofu ya Mungu na anayezingatia mipaka ya dini anaweza kutufaa kuliko asiye na habari na dini. Uchaji Mungu humfanya kiongozi kuwa makini katika maamuzi yake, kwa sababu anajua kuna siku atasimamishwa kwenye mahakama ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kujibu maswali kuhusu matendo yake.

Hiki si kigezo cha lazima na cha msingi sana lakini mbele yako kukiwa na mgombea mcha Mungu na hata anayeamini katika mizimu ni vyema kumpa kipaumbele.

## ELIMU

Pengine si kigezo cha lazima pia lakini katika zama tulizo nazo kiongozi ni vyema awe na elimu ya darasani kwa kiasi fulani.

Imani iliopo ni kwamba maarifa haya ya darasani yatamwezesha kutoa maamuzi yenye busara na kuyatafakari kwa uangalifu kwa kuzingatia hali ya watu wake.

Dunia ya sasa ya utandawazi, dunia ya sayansi na teknoolojia inaweza kumwia vigumu kiongozi asiye soma kwa angalau kidato cha nne kuelewa baadhi ya hoja (concepts).

## HEKIMA NA BUSARA

Kuna watu wana elimu, wana fedha na kama tulivyogusua hapo awali wanaweza kuwa hata wacha Mungu lakini hakujaaliwa hekima na busara na wakati mwingine hii ikitokana na makuzi yao.

Tuwapime viongozi tutakaowachagua kwa uwezo wao wa kutoa maamuzi sahihi, na busara katika kushughulikia changamoto mbalimbali. B

## UVUMILIVU NA SUBIRA

Subira haimaanishi kungoja peke yake bali kwenye muktadha huu ni hali ya uvumilivu wa nafsi.

Kiongozi lazima awe na subira, kuvumilia changamoto. na kuweza kusimamia umma anaouongoza bila kukata tamaa. Subira inahitajika hasa wakati wa matatizo na misukosuko ili aweze kuongoza kwa utulivu na hekima.

## MASHAURIANO

Kiongozi anapaswa pia kupenda kufanya mashauriano na wataalamu pamoja na wananchi wake kabla ya kufanya maamuzi makubwa.

Mashauriano ni njia ya kuhakikisha kuwa maamuzi ya kiongozi yanatokana na maoni ya watu wengi na yanaleta manufaa kwa wote.

Hii ni kinyume na viongozi wababe wanaodhani kwamba akishashika hatamu za uongozi basi yeye ndiye mwenye maarifa na uelewa kuliko watu wote anao waongoza, la hasha.

## KUPATA AU KUJINYONGA

Nimalizie kwa kusema tujaze vizuri hii hundi mpya (blank cheque) iliyoko mbele yetu kwa kuchagua viongozi bora.

Wale waliotuongoza kipindi kilichopita kama tunadhani wanatufaa bado tuwachague tena lakini kama hawakukidhi vigezo kama nilivyovijadili hapo juu ni wakati wa kuwapiga chini.

Hatutakuwa na sababu ya kulakamika huko mbele kama tutachagua viongozi wabaya. Kwa hiyo matarajio pia ni kwamba vyama pia vitapitisha wagombea makini wenye sifa kama nilizozieleza hapo juu.

Tukumbuke pia sheria ya uchaguzi huu imetoa siku saba za mapingamizi ili kila mtu aridhike. Sheria inapotoa nafasi ya mapingamizi, inamaanisha kwamba baada ya wagombea kuteuliwa au kuchukua fomu za kugombea, kunatolewa muda wa siku hizo kwa mtu yeyote aliye na pingamizi dhidi ya mgombea kuwasilisha malalamiko yake.

Pingamizi zinaweza kuhusiana na masuala kama vile sifa za mgombea, kutokubaliana na uteuzi wake, au sababu nyingine zinazoweza kuathiri haki ya mgombea kuwania nafasi husika. Mchakato huu unalenga kuhakikisha uchaguzi unafanyika kwa haki, uwazi, na kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa kisheria.

# Tujikumbushe wimbo wa 'Tazama ramani utaona nchi nzuri'



**Na Mwandishi Wetu**

NAWEZA kusema Tanzania ni nchi yenye upekee hasa kwa kusheheni nyimbo nzuri zenye mrengo wa kukuza uzalendo dhidi ya wananchi wake. Mara nyingi nyimbo zake zimejaa mahaba makubwa ambayo tukifikiria kwa kina sana na angalau kutekeleza asilimia 75 ya kilichoko kwenye nyimbo hizo nchi yetu haiwezi kuwa tena na watu wanaoisema vibaya nje hata kidogo.

Mahaba haya yanayooneshwa kwenye nyimbo zetu hizi pengine yanalenga kutujenga kama vijana hasa kuzidi kuipenda na kuithamini nchi yetu.

Wimbo wa "Tazama ramani utaona nchi nzuri" ni moja kati ya nyimbo hizo nilizogusia hapo juu. Kwa minajili ya kuleta maana katika makala haya naomba kunukuu beti la pili na la tatu; '*Chemchem ya furaha, amani nipe tumaini, Kila mara niwe kwako nikiburudika, Nakupenda sana hata nikakusitiri, Nitalalamika kukuacha Tanzania. Majira yetu haya, yangekuwaje sasa, Utumwa wa nchi, Nyerere ameukomesha X2.*

*Nchi yenye azimio lenye tumaini, Ndiwe peke yako mwanga wa Watanzania, Ninakuthamini hadharani na moyoni, Unilinde nami nikulinde hata kufa. Majira yetu haya, yangekuwaje sasa, Utumwa wa nchi, Nyerere ameukomesha X2.*

Kimsingi wimbo huu unagusia mambo makuu ya kuzingatiwa kwa mstakabali mzima wa taifa letu. Mambo hayo ni pamoja na kudumisha amani, kutoa hali ya matumaini kwa Watanzania masikini walio wengi, ulinzi wa mali asili zetu na kudumisha mapenzi mema kwa nchi yetu yaani uzalendo. Katika muktadha huo, dhana nzima ya kulinda maslahi ya Taifa na wananchi wake ndio jambo la msingi sana katika nchi yoyote ile huru.

Kwa minajili ya kuweka mlolongo mzuri kwa msomaji, Uzalendo ni hali ya mtu kuipenda, kuithamini, kuisitiri na kujitoa kwa ajili ya nchi yake. Mzalendo wa kweli daima anaweka maslahi ya nchi mbele na ya kwake binafsi nyuma.

Kwa maana hiyo, mzalendo ni mtu yeyote mzawa na mwenye kuipenda na kujitoa mhanga na saa nyingine ikibidi kufa kwa ajili ya nchi yake kwa maslahi ya wananchi walo wengi. Uzalendo unabeba dhana nyingi sana ikianzia asili, utamaduni, lugha, siasa, historia, na mambo kadha wa kadha. Dhana zote zikifungwa kwenye dhana kuu ya utaifa.

Kuwa mzalendo ni zaidi ya kuifia nchi yako. Kwa sababu aidha kwa uzembe au kwa ujinga au kwa imani yake mtu aweza kufa lakini kumbe hakuipenda nchi ila kwa matakwa yake binafsi.

Shinikizo la kuifia nchi ni lazima liwe *tunda la uaminifu, upendo wa kujitoa, kuipigania na kuitetea nchi yako.* Wako wazalendo ambao wameitetea nchi yao toka utotoni, ujanani na uzeeni na hawakuifia nchi. Watu wasio wazalendo ni hawa hapa: watu wanaoihujumu nchi kwa kuiba, kutumia rasilimali za nchi vibaya, kuharibu miundombinu, kuweka pesa nje ya nchi, kuisema vibaya nchi na viongozi au watu wake, kushabikia wizi na ufisadi, kuvunja sheria za nchi, kuthamini vitu na mambo kutoka nje.

Kwa hiyo tunapoingia kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, suala la kuchagua viongozi wazalendo ni la kuzingatia sana.

Unaweza kweli ukawa mzawa, mwaminifu, mkweli lakini unakuwa kimya watu wanapoiba na kutumia vibaya rasilimali za nchi, wewe pia sio mzalendo kwa mfano huo. Hii ni pamoja na kuchagua kiongozi ambaye unajua kabisa kwamba hana uzalendo.

Wakati wa kupigania uhuru wa nchi hii, kilichokuwa kinawaongoza na kuwasukuma wapigania uhuru ni uzalendo. Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere na wenzie walikuwa na uzalendo wa dhati kabisa kabisa kupigania utaifa na kuulinda utaifa wetu japo tu kwa njia ya amani.

Wakati huo lengo kubwa lilikuwa ni kutoa nchi yetu chini ya utawala wa mkoloni na kuleta maendeleo kwa Watanganyika na baadae Watanzania wote kwa ujumla.

Kwamba haikutosha kupata uhuru tu bali kuwaletea Watanzania mapinduzi ya kimaendeleo.

Mapinduzi haya yalichukuliwa kama vita ya kulikomboa taifa kiuchumi. Maneno haya yalithibitishwa kwenye sehemu ya tatu ya Azimio la Arusha yanayosema '*TANU ina vita vya kulitoa Taifa letu katika hali ya unyonge na kulitia katika hali ya nguvu; vita vya kuwafanya wananchi wa Tanzania (na wananchi wa Afrika) watoke katika hali ya dhiki na kuwa katika hali ya neema. Tumeonewa kiasi cha kutosha, tumenyonywa kiasi cha kutosha, na tumepuuzwa kiasi cha kutosha. Unyonge wetu ndio uliotufanya tuonewe, tunyonywe, na kupuuzwa. Sasa tunataka mapinduzi; mapinduzi ya kuondoa unyonge ili tusionewe tena, tusinyonywe tena'.*

Baada ya miaka ya 60 tangu nchi yetu imepata uhuru, maneno haya yamekuwa yakitumiwa mara nyingi kwa kutamkwa au vitendo na Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Pombe Magufuli na hata Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika Awamu ya Sita.

Rais Samia amefanya mengi na kuja na miradi na mikakati lukuki ili kuiondoa nchi yetu na wananchi kwenye unyonge.

Hata bila kutamka, kimsingi amerejelea kwenye misingi ya azimio la Arusha?

Ni wazi kabisa kabisa kwamba Rais anataka kuwatoa Watanzania walio wengi katika dimbwi la umaskini.

Katika kipindi cha miaka mitatu ya awali Rais Samia amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuimarisha heshima ya Taifa letu ndani na nje hususani kupaisha diplomasia ya uchumi, japo ni wazi kwamba wasioitakia mema nchi yetu hawapendi sana.

Kwa kiasi kikubwa amedhihirisha pasi na shaka kwamba aliyasoma na kuyashika vyema maneno ya Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere.

Swali lililo kwenye wimbo tajwa hapo awali "*Majira yetu haya, yangekuwaje sasa?* anajitahidi kila uchao kulijibu kwa kusimamia rasilimali za Watanzania.

Kama Rais asingesimamia vyema miradi ya kimkakati Kama reli ya kisasa (SGR) na Bwawa la kuzalisha Umeme la Julius Nyerere, kama asingeleta wawekezaji kuboresha Bandari yetu bila kukata tamaa licha ya maneno maneno mengi ya 'makhulultabi' Watanzania tungekuwa wapi?

Bila kuboresha miundombinu nchi ingekuwa wapi? Kama asingeboresha zahanati tungekuwaje? Na kama asingetoa elimu bure na mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu hali ingekuwaje?

Maswali haya na mengineyo mengi ambayo hata Baba wa Taifa aliyasisitiza mara kwa mara wakati wa uteuzi wa mgombea urais kutoka chama tawala, yanajibiwa vyema na Dk. Samia katika kipindi hiki cha utawala wake.

Pamoja na kwamba amejitahidi kufanya hayo bado kuna wanaoona kwamba anakosea. Kila mara wamekuwa wa kumkosoa hasa kwa vihoja visivyo na mashiko. Kimsingi siwashangai kwa kuwa hata wakati wa kupigania Uhuru kuna walioona kwamba Baba wa Taifa alikuwa anakosea. Haya aliyathibitisha wakati wa majadiliano na mwandishi wa Habari, Saeed Naqvi kufuatia swali lake (ambalo sitanukuu); Baba wa Taifa alisema "*wakati tunapigania Uhuru kuna waliosema kwa nini tunafanya hivyo? Walidai hatuna chochote kuendesha nchi. Lakini ilitubidi kupigania Uhuru, tusingekubali kuendelea kuteseka. Hata sasa wapo wenye mawazo ya kutaka mataifa makubwa yaendelee kututawala na hivyo watafanya kila njia kutukatisha tamaa."*

Hili tulilishuhudia wakati wa uchaguzi mkuu uliopita na pengine kabla ya hapo ambapo baadhi ya wanaharakati wanaojiita wanasiasa walipoamua kuhama nchi na kuisema vibaya.

Oktoba 14 tuliadhimisha miaka 25 tangu kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere na miaka 60 ya Mwenge wa Uhuru na hivyo tunapoadhimisha haya ni vyema kukumbushana juu ya uzalendo kwa maslahi mapana ya Taifa letu na kuungana na viongozi wetu kulinda maslahi ya Taifa letu lakini wakati huo huo kuhakikisha nyimbo zetu za kizalendo zinaimbwa na kila mmoja wetu.

Na Mwsandishi Wetu



# Nyie vijana, hizi ndizo sifa za Mwalimu Nyerere

Oktobva 14, 2024, Taifa liliadhimisha miaka 25 tangu kuondoka duniani kwa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Mengi yameelezwa kuhusu Mwalimu Nyerere kuelekea kilele cha kumbuki yake lakini imenipendeza kukusanya baadhi ya Sifa za Mwalimu Nyerere kwa ajili ya vijana kwani inasemekana Watanzania vijana, zaidi ya asilimia 60 hawakuwahi kumwona Mwalimu Nyerere.

Tunapoelekea kwenye chaguzi zetu, tukianza na uchaguzi wa serikali za mitaa, ni vyema Watanzania hasa vijana wanaofikiria kuwania uongozi kujifunza kutoka kwa Mwalimu.

**1. KIONGOZI WA UADILIFU**

Mwalimu Nyerere alikuwa mtu wa maadili ya hali ya juu na aliamini sana katika uadilifu wa kisiasa na kijamii. Aliishi kwa mfano, akiepuka matumizi mabaya ya madaraka na rasilimali za umma. Hata baada ya kustaafu urais, aliendelea kuishi maisha ya kawaida bila kujitajirisha kutokana na nafasi yake ya uongozi.

**2. MFUASI WA UJAMAA**

Nyerere alianzisha sera ya Ujamaa, falsafa iliyokuwa inahimiza usawa wa kijamii na umiliki wa pamoja wa rasilimali za uchumi. Kupitia mpango wa Azimio la Arusha (1967), alihimiza maendeleo ya vijiji vya ujamaa, ambako watu wangeishi pamoja na kushirikiana katika shughuli za kilimo na uzalishaji. Ingawa sera hii haikufanikiwa kama alivyotarajia, nia yake ilikuwa kusaidia kujenga uchumi wa ndani unaotegemea ushirikiano badala ya ukoloni mamboleo.

**3. MPENDA ELIMU**

Mwalimu Nyerere alikuwa mwalimu kabla ya kuwa mwanasiasa na ndio maana hadi sasa tunamwita Mwalimu. Aliona elimu kama nyenzo muhimu ya kuwakomboa watu kiuchumi na kiakili.

Alipendekeza mfumo wa elimu unaojikita katika mahitaji ya jamii na alihimiza kwamba watu wapate elimu bora ili waweze kujitegemea. Aliweka mkazo katika elimu ya watu wazima, elimu ya msingi kwa wote, na alianzisha mpango wa kujenga shule nyingi vijijini.

**4. MTETEZI WA UMOJA WA AFRIKA**

Mwalimu Nyerere alikuwa mtetezi mkubwa wa umoja wa Afrika. Alikuwa miongoni mwa waanzilishi wa Shirikisho la Afrika Mashariki na alishiriki kikamilifu katika uundaji wa Umoja wa Afrika (OAU) ambao sasa unajulikana kama Umoja wa Afrika (AU).

Aliamini kuwa Afrika lazima iungane ili kukabiliana na changamoto za kiuchumi, kisiasa, na kijamii zinazokumba bara hilo. Hakuogopa kusimama kidete kwa ajili ya uhuru wa mataifa mengine ya Afrika yaliyokuwa bado hayajajikomboa, akitoa msaada mkubwa kwa wapigania uhuru barani kote, kama vile katika nchi za Msumbiji, Zimbabwe, Namibia na Afrika Kusini.

**5. BUSARA NA MVUMILIVU**

Nyerere alikuwa na tabia ya upole, busara, na uvumilivu katika kushughulikia changamoto mbalimbali. Ingawa si kila mtu alikubaliana na sera zake, aliendelea kushikilia imani yake kwamba maendeleo ya kweli yanapaswa kuja kwa njia ya haki na usawa.

Tabia yake ya kujadiliana kwa amani ilionekana hata alipokubali kuondoka madarakani bila kulazimishwa, akiachana na utawala kwa hiari mnamo mwaka 1985, jambo ambalo lilionyesha ukomavu wake wa kisiasa na demokrasia.

Mwaka 1992 alishauri nchi kwenda kwenye utawala wa vyama vingi ingawa kura za maoni zilionesha kwamba aslimia 80 ya Watanzania bado walikuwa wanataka mfumo wa chama kimoja. Busara zake zilichangia sana nchi kuingia kwenye mfumo wa vyama vingi.

**6. MWANAFALSAFA NA MWANDISHI**

Nyerere alikuwa mwanafalsafa na msomi aliyependa kujadiliana masuala ya kina kuhusu uongozi na jamii. Aliandika makala, hotuba na vitabu vingi vinavyohusu siasa za Afrika, ukoloni, na ujamaa. Pia alitafsiri baadhi ya maandiko ya kifalsafa ya dunia kama vile maandiko ya William Shakespeare ("The Merchant of Venice" na "Julius Caesar") na vitabu vya dini kama Biblia kwa Kiswahili.

**7. MZALENDO NA MWAFRIKA WA KUJIVUNIA**

Nyerere alikuwa mzalendo wa kweli aliyepigania uhuru wa Tanganyika kutoka kwa Wakoloni wa Kiingereza, lakini hata baada ya uhuru, alihimiza heshima kwa mila na desturi za Kiafrika. Alitaka kujenga taifa lenye utambulisho wake, linalojivunia tamaduni zake na linalojitegemea kiuchumi. Alisaidia sana kutokomeza ukabila na kunyanyua Lugha ya Kiswahili.

**8. MPENDA AMANI**

Nyerere alikuwa mpatanishi wa kimataifa, akisaidia kutatua migogoro mbalimbali barani Afrika na duniani kote. Aliwahi kuwa mpatanishi katika mzozo wa Burundi na alikuwa na msimamo wa kutoegemea upande wowote wakati wa vita baridi, akihimiza sera ya kutofungamana na upande wowote (Non-Alignment).

Kwa ujumla, Nyerere alikuwa kiongozi anayeheshimika sana kwa hekima yake, uzalendo, na kujitolea kwa maendeleo ya watu wake na bara la Afrika kwa ujumla. Licha ya changamoto kadhaa zilizokumba sera zake, alibaki kuwa kipenzi cha wengi na mfano wa kuigwa kwa viongozi wengi wa Afrika.

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alizaliwa tarehe 13 Aprili 1922 katika kijiji cha Butiama, mkoani Mara, Tanzania. Alikuwa mtoto wa chifu wa kabila la Wazanaki,. Chifu Burito Nyerere.

Mwalimu Nyerere alipata elimu yake ya awali katika shule ya Mwisenge, Musoma Mjini kabla ya kuendelea na masomo ya sekondari katika Shule ya Tabora Boys. Alipata nafasi ya kusoma Chuo Kikuu cha Makerere, Uganda, ambako alihitimu kama mwalimu. Baadaye alisomea shahada ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Edinburgh, Scotland, akiwa mmoja wa Waafrika wachache waliopata elimu ya juu katika kipindi hicho.

Baada ya kurejea Tanganyika mwaka 1952, Nyerere alifundisha katika shule ya St. Mary's Tabora (Sasa Milambo High School) na Francis' College sasa Pugu Sekondari lakini harakati zake za kisiasa zilianza kukua alipojiunga na chama cha Tanganyika African Association (TAA).

Mnamo mwaka 1954, alibadilisha TAA kuwa Chama cha Tanganyika African National Union (TANU), ambacho kiliongoza harakati za kudai uhuru wa Tanganyika.

Nyerere alikuwa mstari wa mbele katika kupigania uhuru kwa njia za amani, na jitihada zake zilifanikiwa mnamo Desemba 9, 1961, wakati Tanganyika ilipopata uhuru. Alikuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Tanganyika na baadaye akawa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Tanganyika mwaka 1962. Baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964, Nyerere akawa Rais wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wakati wa utawala wake, Nyerere alianzisha sera ya Ujamaa, iliyolenga kujenga jamii yenye usawa wa kijamii na kiuchumi kupitia vijiji vya ushirika. Pia alitetea haki za Waafrika na kusaidia harakati za ukombozi barani Afrika, hasa nchi kama Msumbiji, Zimbabwe, na Afrika Kusini.

Mwalimu Nyerere alijiuzulu urais mwaka 1985 kwa hiari na akaendelea kuwa sauti muhimu ya hekima barani Afrika. Aliaga dunia tarehe 14 Oktoba 1999 huko London, Uingereza, kutokana na ugonjwa wa saratani ya damu. Anaendelea kukumbukwa kama Baba wa Taifa na mmoja wa viongozi mashuhuri zaidi kuwahi kutokea barani Afrika.

Vijana mnaogombea uongozi, mna nafasi ya kuwa kama Nyerere.



## Kurunzi

Na Dk. Reubeni Lumbagala | 0620 800 462

# Ubia kwenye viwanda vya saruji utachagiza maendeleo nchini



Ushirikiano kati ya serikali na sekta binafsi (Public and Private Partnership-PPP) ni jambo nyeti na muhimu na limeshaelezwa sana na hata mimi nimeshalieleza kwenye makala zangu na nitaendelea kulieleza kutokana na umuhimu wake katika kuharakisha maendeleo nchini.

Hii inatokana na ukweli ulio dhahiri kuwa kama serikali na sekta binafsi zitaunganisha nguvu ya pamoja katika kutekeleza miradi na programu mbalimbali, wananchi watapata maendeleo kwa haraka zaidi.

Katika muktadha huo, Chuo Cha Elimu ya Biashara (CBE) kimeshafanya ubunifu wa kushirikiana na sekta binafsi na kufanikisha ujenzi wa mabweni ili kupunguza tatizo la wanafunzi wa chuo hicho kuishi nje ya chuo kutokana na ukosefu wa mabweni ya kutosha ndani ya kampasi.

Kama chuo kingesubiri pesa kutoka serikalini bila shaka hatua hii ya kuharakisha upatikanaji wa mabweni ingechukua muda sana.

Wiki iliyopita nilizungumzia ubia kati ya serikali na sekta binafsi, nikijielekeza katika mpango wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA) kushirikisha sekta binafsi katika kuboresha huduma za vivuko, mitambo na karakana ili wananchi waweze kupata huduma bora na kuchochea maendeleo.

Katika eneo jingine muhimu ambalo serikali imeipa kipaumbele suala la ubia kati yake na sekta binafsi ni ujenzi wa viwanda vya saruji. Viwanda hivi ambapo kimoja kiko Mbeya kinaboreshwa na kingine Tanga kinajengwa ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi kwa kuongeza ajira na kukuza sekta za ujenzi, makazi na biashara.

Serikali ambayo moja ya kazi yake kubwa ni kuhakikisha uwepo wa huduma muhimu kwa wananchi, inayo wajibu wa kuhakikisha bidhaa ya saruji inapatikana kwa bei nafuu ili kuwawezesha wananchi na taasisi nyingine kuweza kumudu kununua bidhaa hiyo muhimu ili kufanikisha ujenzi wa miradi mbalimbali na makazi ya watu. Kumbuka moja ya mahitaji ya msingi ya mwanadamu ni makazi.

Mkakati mmojawapo muhimu utakaowezesha bidhaa ya saruji kupatikana kwa bei nafuu nchini ni kuongeza idadi ya viwanda vinavyozalisha saruji katika mikoa na kanda mbalimbali nchini na hasa kwa kuzingatia kwamba sehemu kubwa ya malighafi ya saruji inapatikana nchini. Wingi wa viwanda utaongeza upatikanaji wa bidhaa na hivyo kuifanya bidhaa hiyo ipatikane kwa bei nafuu.

Uwepo wa viwanda vingi vya saruji nchini itawezesha sekta ya ujenzi na makazi kupiga hatua kubwa na hivyo kuchangia maendeleo.

Vilevile, ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo kama vile barabara, shule, hospitali, maji, masoko, ofisi kutaja kwa uchache inatumia saruji nyingi hadi ukamilishaji wake, hivyo basi, upatikanaji wa saruji nchini na kwa bei nafuu utafanikisha utekelezaji wa miradi hii kwa gharama nafuu na kukuza maendeleo.

Nguvu ya ubia kati ya serikali na sekta binafsi kupitia kampuni ya Amsons umeonekana katika dhamira ya kupanua kiwanda cha saruji mkoani Mbeya ambapo utagharimu Dola za Marekani milioni 130 na ujenzi wa kiwanda kipya mkoa wa Tanga, ambao utagharimu Dola za Marekani Milioni 190 kwa pamoja miradi hii miwili itagharimu Dola za Marekani Milioni 320 sawa na bilioni 850 za Tanzania.

Oktoba 15, 2024, Msajili wa Hazina Nehemiah Mchechu katika mkutano na waandishi wa habari alisisitiza kuwa kupitia uwekezaji huu mkubwa, uzalishaji katika kiwanda cha saruji Mbeya utaongezeka kutoka tani 1,000 hadi 5,000 kwa siku na kiwanda kipya mkoani Tanga kitazalisha tani 5,000 kwa siku, na kufanya uzalishaji katika viwanda hivi viwili kuwa tani 10,000 kwa siku na kwa mwaka vitazalisha tani milioni 4.2 ambapo awali uzalishaji kwa mwaka ulikuwa ni tani milioni 1.1 (ongezeko la tani nilioni 3.1 kwa mwaka).

"Mahitaji ya saruji nchini ni makubwa kutokana na ujenzi wa miundombinu na uwekezaji unaofanywa na serikali, wawekezaji wakiongezeka bei ya saruji itapungua. Tunakwenda kufanya uwekezaji ili kukamata vizuri soko la Tanzania na soko la nchi jirani kama vile Zambia, Malawi na DRC (Congo). Tumeshafanya maamuzi ya msingi tunakwenda kuwekeza na baada ya miaka miwili au mitatu tutakuwa katika hatua nzuri," amesema Mchechu.

Ni muhimu mahitaji ya bidhaa yanapoongezeka kuja na ubunifu wa kuongeza uzalishaji ili kupunguza ongezeko la bei ya bidhaa hiyo. Katika mahitaji matatu muhimu ya binadamu ambayo ni chakula, mavazi na malazi, hitaji la malazi linategemea sana matumizi ya saruji. Hivyo basi, upatikanaji wa saruji ya bei nafuu utawezesha wananchi wengi kufikia ndoto zao za kumiliki nyumba ambapo ni hitaji muhimu katika maisha ya mwanadamu chini ya jua.

Faida za viwanda hivi ni nyingi. Mosi, kuongezeka kwa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zipatazo 12,000.

Pili, serikali itakusanya kodi, na hivyo kuchangia ongezeko la makusanyo ya kodi yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Tatu, kukua kwa biashara ya uuzaji wa saruji ndani na nje ya nchi. Aidha, wananchi wana fursa ya kufungua migahawa kuzunguka viwanda hivi na kuuza bidhaa za vyakula, vitafunwa na vinywaji kwa wafanyakazi wa viwanda hivi.

Vilevile, wamiliki wa vyombo vya usafiri kama vile malori watapata fursa ya kusafirisha bidhaa hiyo ndani na nje ya nchi na hatimaye kuchangia maendeleo. Madereva ya bodaboda watapata abiria ambao ni wafanyakazi wa viwanda hivi pindi waendapo kazini au kurudi nyumbani.

Bandari ya Tanga kwa upande wake inayo fursa ya kusafirisha saruji kwa njia ya maji kwenda maeneo mbalimbali kama vile Zanzibar, Dar es Salaam na nchi nyingine. Hii itasaidia kuchechemua ajira, biashara, uchumi na kuongeza pato la Taifa.

Nihitimishe kwa kuwashauri wakandarasi wanaotekeleza miradi hii miwili wazingatie ubora na kasi katika ujenzi kwani mahitaji ya saruji ni makubwa sana kutokana na wingi wa shughuli na miradi inayohitaji saruji ndani na nje ya Tanzania.

Serikali iendelee kutumia ubia baina yake na sekta binafsi katika ujenzi wa viwanda vingine vya saruji nchini ili kuwawezesha wananchi kuwa na makazi bora na kufanikisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayohitaji saruji ili kuifanikisha.

*Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.*

## UCHAGUZI WA MAREKANI:

# Trump kutoka mfanyabiashara wa majengo hadi mwanasiasa





MIAKA mingi nyuma kabla ya kugombea mara tatu mfululizo kuwania Urais wa Marekani, Donald Trump (78), alikuwa bilionea mwenye mbwembwe nchini Marekani.

Maisha ya tajiri huyo wa majengo huko New York, yalikuwa kwenye magazeti ya udaku na runinga katika miongo kadhaa kabla ya mbio zake zisizotarajiwa za mwaka 2015 -2016 kuingia Ikulu ya White House.

Jina lake na mtindo wake wa kampeni, vilimsaidia kuwashinda wanasiasa wenye uzoefu, lakini enzi iliyojaa utata ilimfanya aondolewe madarakani kwa kura baada ya muhula mmoja.

### MRITHI WA BABA YAKE

Trump ni mtoto wa nne wa mfanyabiashara wa majengo huko New York, Fred Trump.

Alipelekwa katika shule ya kijeshi akiwa na umri wa miaka 13 alipoanza utovu wa nidhamu shuleni.

Baada ya kupata shahada ya awali kutoka Chuo Kikuu cha Pennsylvania, alionekana kuwa ndiye wa kumrithi baba yake, wakati kaka yake mkubwa, Fred, alipochagua kuwa rubani.

Fred Trump alifariki dunia akiwa na umri wa miaka 43 kutokana na ulevi wa kupindukia, jambo ambalo Trump anasema lilimpelekea kuepuka pombe na sigara maisha yake yote.

Trump anasema aliingia kwenye biashara ya majengo akiwa na mkopo wa Dola za Kimarekani milioni moja kutoka kwa baba yake kabla ya kujiunga na kampuni hiyo.

Alisaidia kusimamia miradi ya makazi ya baba yake katika mitaa ya Jiji la New York na kuchukua udhibiti wa kampuni hiyo ambayo aliipa jina la Trump Organisation mwaka 1971.

Baba yake, ambaye Trump anamtaja kama "msukumo wangu," alifariki dunia mwaka 1999.

### BIASHARA ZA TRUMP

Chanzo cha picha,Getty Images

Chini ya Trump, biashara ya familia ilihama kutoka majengo ya makazi ya kuishi huko Brooklyn na Queens hadi miradi ya Manhattan.

Mtaa maarufu wa Fifth Avenue, ukawa makazi ya ghorofa la Trump Tower, bila shaka ndiyo jengo maarufu la tajiri huyo na nyumba yake kwa miaka mingi.

Na hoteli ya Commodore ikaitwa Grand Hyatt.

Majengo mengine yenye jina la Trump – kama makasino, ghorofa za makazi, viwanja vya gofu na hoteli, yalijengwa pia, huko Atlantic City, Chicago na Las Vegas, India, Uturuki na Ufilipino.

Chanzo cha picha,Getty Images

Kuibuka kwake kuwa maarufu kuliendelea katika ulimwengu wa burudani, kwanza kama mmiliki wa shindano la Miss Universe, Miss USA, na Miss Teen USA, kisha kama mtayarishaji wa kipindi cha NBC The Apprentice.

Trump ameandika vitabu kadhaa, alionekana katika filamu na programu ya kuunga mkono mieleka, na alikuwa muuzaji wa kila kitu kutoka vinywaji hadi tai.

Lakini utajiri wake umeshuka katika miaka ya hivi karibuni. Forbes inakadiria kuwa kwa sasa ana utajiri wa Dola za Kimarekani bilioni nne.

Trump pia ametangaza kufilisika kwa biashara kadhaa kwa nyakati sita tofauti, ikiwa ni pamoja na mradi wa Trump Steaks na Chuo Kikuu cha Trump.

Pia amleficha taarifa zake kuhusu ushuru ili zisichunguzwe, na ripoti ya 2020 ya gazeti la New York Times lilifichua miaka ya kukwepa ushuru wa mapato na upoteaji wa fedha.




### FAMILIA YAKE

Maisha ya binafsi ya Trump yako hadharani. Mke wake wa kwanza, anayejulikana zaidi, ni Ivana Zelnickova, mwanariadha wa Czech na mwanamitindo.

Wamepata watoto watatu - Donald Jr, Ivanka na Eric - kabla ya talaka mwaka 1990.

Kesi yao mahakamani ilikuwa kwenye kurasa za mbele za magazeti ya udaku, na madai ya marehemu Bi. Trump ya kunyanyaswa ambayo baadaye aliyapuuza katika makala ya runinga kuhusu Trump.

Alimwoa mwigizaji Marla Maples mwaka 1993, miezi miwili baada ya kuzaliwa mtoto wao pekee Tiffany. Waliachana mwaka 1999.

### MKE WA SASA

Mke wake wa sasa wa Trump ni mwanamitindo wa zamani wa Slovenia, Melania Knauss.

Walifunga ndoa mwaka 2005 na wana mtoto wa kiume, Barron William Trump, ambaye hivi karibuni ametimiza miaka 18.

Madai ya utovu wa maadili na uchepukaji nje ya ndoa

>> Inaendelea Uk. 19



# Utata wa kifo cha JF Kennedy wa Marekani-6

**Simulizi kuhusu utata wa kifo cha Rais wa 35 wa Marekani John Fitzgerald Kennedy aliyeingia ofisini Januari 20, 1961 hadi alipouawa Novemba 22 mwaka 1963. Ikiwa ni miaka 61 imepita tangu kifo hicho, tumeangalia safari yake ya kutembelea Jimbo la Texas akiwa na malengo kadhaa, kubwa likiwa ni kujiimarisha kisiasa katika jimbo hilo baada ya kutofanya vizuri sana katika uchaguzi uliokuwa umemwingiza madarakani. tulianza kuangalia namna safari yake ilivyotangazwa, maofisa usalama walivyokagua maeneo ya kupita, safari ilipoanza kwa njia ya gari kutoka Kiwanja cha Ndege cha Love Field kuelekea Dallas Trade Mart, katikati mwa jiji la Dallas, Jimbi la Texas pamoja na mpangilio wa magari ulivyokuwa. Wiki iliyopita tuliagalia jinsi alivyopigwa risasi, akakambizwa hospitali na kisha makamu wake, Lyndon Johnson akawa anatakiwa kutangaza rasmi kifo chake ili kuondoa utata. Mwandishi Wetu, HAMID YASSIN anaendelea kuangalia utata kuhusu mtu anayedaiwa kumuua Rais Kennedy, Lee Harvey Oswald kama ni yeye kweli. Kuna utata mwingi kuhusu ushahidi unaotolewa kuhusu mtu huyu.**

Msimamizi wa jengo alimtambulisha Oswald kwa askari kuwa alikuwa ni mfanyakazi wa jengo hilo, hivyo ikambidi polisi amuache Oswald na kuendelea na upekuzi katika floor za juu.

Purukushani yote hii kutoka muda ambao Baker alisikia mlio wa risasi akiwa kwenye msafara wa Rais mpaka kuja kukutana na Oswald ghorofa ya pili ya jengo la Texas School Books Depository, ilichukua kama sekunde 74 mpaka sekunde 90 tu.

Maelezo na mkazo zaidi kwenye 'feature' moja muhimu ya bunduki hizi, telescopic sight.

Bunduki nyingi zilizopo za Mannlicher-Carcano (hata kipindi hicho cha mwaka 1963) hazina Telescopic sight (darubini ya mdunguaji, yaani ile lenzi ambayo sniper anachungulia kupata muono mzuri wa shabaha yake).

Lakini bunduki inayodaiwa kutumiwa na Oswald ilikuwa na telescopic sight. Hii ina maana kwamba eidha aliifanyia modifications au alihangaika kupata model chache za Carcano zilizozalishwa miaka ya 1940s.

Kuna kitu ambacho watumiaji wengi wa silaha watakuwa wanakifahamu, kinaitwa GSR au wengine wanaita CDR (Gunshot Residue au Cartridge Discharge Residue).

Hili ni kama unga au vumbi fulani jembamba sana linatoka ukifyatua risasi na mara nyingi huwezi kuliona.

Vumbi hili linatokana na 'propellant' ya risasi ndani ya bunduki pale inapofyatuliwa, pia vipande vidogo vidogo sana (particles) za risasi na catridge ikifyatuka.

Kitaalamu, GSR inaruka futi 3 mpaka 5 kutoka bunduki ilipofyatuliwa, kwa maana ya kwamba mtu anayefyatua bunduki hii ni lazima atarukiwa na 'vumbi' hili la GRS na vumbi hili huwa linakaa mwilini kwa mfyatuaji risasi kwa masaa matatu mpaka sita kitegemea na aina ya silaha iliyotumika.

Katika uchunguzi wa matukio ya uhalifu kwa kutumia silaha kuna kipimo kinaitwa 'Paraffin Test'.

Kipimo hiki huwa kinapima uwepo wa GRS katika nguo na mwili wa mtu ambaye anahisiwa kutumia hiyo silaha katika tukio hilo mahususi.

Kipimo kikileta majibu positive, hii maana yake ni kwamba mtu huyo alifyatua hiyo risasi, au alikuwa karibu muda ambao risasi ilipofyatuliwa au aliigusa risasi silaha muda mfupi baada ya kufyatuliwa.

Majibu ya kipimo yakija negative, hii ina maana kwamba mtu huyo hakufyatua risasi, au hakuwa karibu muda ambao risasi ilifyatuliwa au hakuigusa silaha baada ya kifyatuliwa.

Turudi kwenye ninachojaribu kueleza, kwa mujibu wa taarifa ya makao makuu ya Polisi Dallas ambapo Oswald alishikiliwa, alipokuwa hapo kituoni alifanyiwa 'Paraffin Test'.

Ajabu ni kwamba majibu yalikuja 'negative!!'

Maana yake ni kama nilivyoeleza hapo juu, majibu haya hasi yanamaanisha kuwa mtu huyu hakufyatua risasi, na hakuwa karibu na silaha wakati inafyatuliwa na wala hakuigusa baada ya kufyatuliwa.

Hii ina maana gani? Warren Commission na serikali hawakuiona hii ripoti ya Polisi?

Jibu ni kwamba waliiona na wakaja na "majibu" yao;

Kwamba, kwenye ripoti ya Warren Commission wanaeleza kuwa, walimhoji mama anayeitwa Earlene Roberts. Huyu ni yule mama wa usafi katika jengo ambalo kulikuwa na chumba cha Oswald anapoishi.

Warren Commission wanadai kuwa mama huyu aliwaeleza kuwa, alimwona Oswald akirudi kwake na kuondoka tena baada ya kama dakika tatu au nne na alipoondoka alikuwa amevaa nguo nyingine tofauti na zile za awali alizokuja nazo.

Kwa hiyo Warren Commission wakatumia ushahidi huu kuhitimisha swali la kwa nini majibu ya 'Parrafin Test' ya Oswald yalikuja negative.

Ufafanuzi wao ni kwamba nguo alizozivaa wakati anapimwa hicho kipimo hazikuwa zile ambazo alizivaa wakati anafyatua risasi na hata baada ya kupekuliwa alipokuwa anaishi na nguo za awali kupatikana tayari muda ulikuwa umepita kuwezesha kipimo kubashiri uwepo wa GSR.

Lakini huu ni ukweli nusu ambao unapotoshwa kwa makusudi au kwa bahati mbaya.

Inaelezwa kwamba, bunduki inayodaiwa kutumiwa na Oswald ina telescopic sight (darubini ya kudungulia). Maana yake kwamba mtumiaji lazima ainame juu ya bunduki ili aweze kuchungulia kutumia telescopic sight.

Maafisa wote wa FBI (Marksmen) ambao walitumiwa kwenye uchunguzi wa miaka ya hivi karibuni kutafiti juu ya GSR kwa kutumia bunduki ile ile inayodaiwa ilitumiwa na Oswald ikiwa na telescopic sight, katika vipimo vya Parrafin wote walikutwa na kiwango kikubwa cha GSR usoni na hasa hasa mashavuni.

Kwa hiyo, maelezo ya kuwa Oswald alibadili nguo ndio maana majibu ya 'Parrafin Test' yakaonyesha negative yanakuwa hayajitoshelezi sana.

*Itaendelea*

# Trump kutoka mfanyabiashara wa majengo hadi mwanasiasa



>> Inatoka Uk. 17

yamemwandama Trump.

Mapema mwaka huu, majaji wawili tofauti walimpata Trump na hatia ya kumkashifu mwandishi E Jean Carroll katika juhudi za kukanusha shitaka la unyanyasaji wa kijinsia.

Aliamriwa kumlipa Dola milioni 88, lakini amekata rufaa.

Trump pia alipatikana na hatia kwa makosa 34 ya kughushi rekodi za biashara katika malipo ya pesa za kumnyamazisha mwigizaji wa filamu za ngono Stormy Daniels, juu ya madai ya kutoka naye nje ya ndoa mwaka 2006.

**MGOMBEA URAIS**

Chanzo cha picha,Getty Images

Katika mahojiano ya 1980, Trump akiwa na umri wa miaka 34, anaelezea siasa ni "maisha duni" na kusema "watu wenye uwezo" huchagua ulimwengu wa biashara.

Kufikia mwaka 1987, alianza kueleza hamu ya kuwania urais.

Alichunguza uwezekano wa kuingia katika mbio za urais mwaka 2000 na kupitia Chama cha Reform na cha Republican mwaka 2012.

Trump alikuwa miongoni mwa waumini wa nadharia ya "birtherism," nadharia inayohoji iwapo Barack Obama alizaliwa Marekani.

Hakukubali kuwa nadharia hiyo ni ya uwongo hadi 2016, lakini hakuwahi kuomba msamaha.

Juni, 2015 Trump alitangaza rasmi mbio za Ikulu ya White House. Katika hotuba ya awali, alionyesha utajiri wake na mafanikio ya biashara; akaishutumu Mexico kwa kuleta dawa za kulevya, uhalifu na wabakaji Marekani; na, kuahidi kuifanya nchi hiyo kulipia ujenzi wa ukuta katika mpaka.

Mijadala na sera zilizojaa utata vilivutia wafuasi na wakosoaji kwa kiwango sawa, pamoja na kufuatiliwa na vyombo vya habari.

Chini ya kauli mbiu ya 'Make America Great Again', aliwashinda wapinzani wake katika Chama cha Republican kwa urahisi na kukabiliana na Hillary Clinton wa Democrat.

Kampeni zake zilikumbwa na utata, ikiwa ni pamoja na kuvuja kwa kanda ya sauti yake akijigamba kuhusu unyanyasaji wa kijinsia na alikuwa nyuma katika kura za maoni wakati wote wa uchaguzi mkuu.

Lakini Trump ndiye aliyecheka mwisho dhidi ya wachambuzi na wadadisi kwa ushindi wake wa kushangaza dhidi ya Hillary. Aliapishwa kuwa rais wa 45 wa nchi hiyo tarehe Januari 2017.



**RAIS**

Kutoka saa chache tu tangu aanze kazi, vituko vikaibuka akitoa matangazo rasmi kwenye Twitter (sasa X) na kugombana waziwazi na viongozi wa kigeni.

Alijiondoa katika mikataba ya mabadiliko ya tabianchi na biashara, akapiga marufuku watu kutoka nchi saba zenye Waislamu wengi kuingia Marekani, akaweka vikwazo vingine vikali katika uhamiaji, akaanzisha vita vya kibiashara na China, akatekeleza sera ya kupunguza kodi na kurekebisha uhusiano wa Mashariki ya Kati.

Kwa takriban miaka miwili, mchunguzi maalumu alichunguza madai ya kula njama ya timu ya kampeni ya Trump ya 2016 na Urusi.

Watu 34 walikabiliwa na mashitaka ya uhalifu kuhusu masuala kama vile udukuzi wa kompyuta na uhalifu wa kifedha, lakini siyo Trump.

Baadaye, Trump akawa Rais wa tatu wa Marekani katika historia kushtakiwa, kwa tuhuma za kuishinikiza serikali ya kigeni kufichua machafu ya mpinzani wake, Joe Biden.

Alipigwa kura ya kutokuwa na imani naye na Bunge linaloongozwa na Democrat, lakini kura hiyo haikupita katika Seneti inayoongozwa na Republican.

Mwaka wa uchaguzi wa 2020, ulitawaliwa na janga la Uviko 19.

Alikabiliwa na ukosoaji mkubwa kwa namna alivyoshughulikia janga hilo wakati Marekani ikiongoza kwa vifo na maambukizi na alitoa maoni yenye utata, pale alipopendekeza, ikiwa virusi hivyo vinaweza kutibiwa kwa kudunga sindano mwilini ya kuharibu virusi.

Alilazimika kuchukua mapumziko ya kampeni zake Oktoba baada ya mwenyewe kugunduliwa na Covid-19.

Ingawa alipata kura milioni 74 zaidi ya rais mwingine yeyote wa Marekani aliye madarakani, lakini alipoteza kinyang'anyiro hicho kwa Biden kwa zaidi ya kura milioni saba.

Kuanzia Novemba, 2020 hadi Januari 2021, alitoa madai kuwa kura zimeibiwa na udanganyifu mkubwa wa uchaguzi umefanyika, madai ambayo hayakuthibitishwa katika kesi zaidi ya 60 kortini.

Alikataa kukubali matokeo na alikusanya wafuasi wake mjini Washington Januari 6, akiwataka wakusanyike kwenye majengo ya Bunge wakati ushindi wa Biden ukithibitishwa rasmi na Congress.

Mkusanyiko huo ulizua ghasia zilizowaweka wabunge na makamu wake, hatarini na kusababisha kupigiwa kura ya kutokuwa na imani naye tena kwa mara ya pili.

Trump alipenya tena katika Seneti, ingawa kwa kura chache zaidi.

Vitendo vyake siku hiyo ndiyo kiini cha kesi mbili za jinai za sasa.

**MBIO ZA KURUDI IKULU**

Maisha ya kisiasa ya Trump yalionekana kama yamekufa baada tukio la Capitol.

Wafadhili na wafuasi waliapa kutomuunga mkono tena na hata washirika wake wa karibu walimkataa hadharani.

Hakuhudhuria kuapishwa kwa mrithi wake na akaihamishia familia yake Florida.

Lakini akiwa na jeshi la wafuasi watiifu, aliendelea kuwa na ushawishi mkubwa katika Chama cha Republican.

Urithi wa urais wake uliibuka tena baada majaji watatu wa mrengo wa kulia ambao aliwateua kwenye Mahakama ya Juu walipoondosha sheria ya takribani miaka 50 ya haki ya kitaifa ya utoaji mimba.

Licha ya kulaumiwa kwa matokeo mabaya ya chama cha Republican katika uchaguzi wa katikati ya muhula wa 2022, Trump alitangaza kuwania tena urais na kisha akawa kinara wa chama hicho.

Zaidi ya wagombea 10, akiwemo Makamu wake wa zamani wa Rais, walishindana naye, lakini akashinda kwani Trump alikwepa mijadala nao na kuelekeza hasira zake kwa Biden.

Trump alianza mbio za kuelekeza uchaguzi mkuu akikabiliwa na mashitaka 91 ya uhalifu katika kesi nne za jinai, lakini mkakati wake wa kuchelewesha kesi hizo umefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Kesi tatu sasa hazitasikilizwa hadi uchaguzi upite na hukumu ya kesi nyingine huko huko New York imecheleweshwa hadi mwishoni mwa Novemba, mwaka huu.

Julai 13, mwaka huu, kijana mwenye bunduki mwenye umri wa miaka 20, alijaribu kumuua Trump wakati wa mkutano wa kampeni huko Butler, Pennsylvania.

Thomas Matthew Crooks, alifyatua risasi nane kutoka juu ya paa la karibu, na kumjeruhi Trump katika sikio lake la kulia kabla ya mshambuliaji huyo kuuawa.

Siku kadhaa baadaye, kwenye Kongamano la Kitaifa la Republican, chama hicho kilimsifu na kumtawaza rasmi kuwa mgombea urais wa Republican kwa mara ya tatu mfululizo, na kuanzisha pambano la marudiano dhidi ya Biden.

Tangu Biden ajiuzulu na kumuunga mkono Naibu wake, Kamala Harris, Trump amejaribu kumfungamanisha na kushindwa kwa utawala wa Biden.

Trump amewaambia wafuasi wake kwamba Novemba 5, mwaka huu, tarehe ya uchaguzi wa Marekani, itakuwa tarehe muhimu zaidi katika historia ya nchi yao.

BBC.

# Usiku ulikuwa mfupi enzi za Marquiz, OSS

## ● Historia ya muziki nchini hainogi bila 'Sikinde', 'Msondo'
## ● 'Sagarumba', 'Paselepa', 'Njata' zilinyima watu usingizi

**Na Hamid Yassin**

IJUMAA iliyopita wadau wa muziki wa dansi waliirudisha jukwaani bendi kongwe ya muziki wa dansi ya Orchestra Marquiz iliyopotea miaka kadhaa iliyopita.

Maquiz walitumbuza pale kwenye Ukumbi wa Bwalo la Maofisa wa Polisi Osterbay. Hakika wametukumbusha mbali sana sisi wadau wa muziki huu wa dansi.


Acha huko miaka ya nyuma zaidi, isipokuwa kwa faida ya wengi, nizungumzie muziki ulivyokuwa nchini hususan kwenye miaka ya 1970 ambapo nchi, na zaidi Jiji la Dar es Salaam, ambako watu waliokunywa maji ya muziki, walikuwa hawawezi kupata lepe la usingizi pasipo kuzishuhudia bendi za Orchestra Marquiz du Zaire (OMACO) na Orchestra Safari Sound (OSS), ilhali wanazi wa bendi za Mlimani Park 'Sikinde' na OTTU Jazz 'Msondo' nao wakisababisha ubishi wa kuuana.

Wakati huo, gumzo kubwa lililokuwa halikauki midomoni mwa wapenzi wa muziki, ni kuhusu bendi mbili za Kicongo (zamani ikiitwa Zaire), Marquiz du Zaire iliyokuwa na utitiri wa mitindo, sawa na OSS ambayo nayo katika uwepo wake, ilibadilisha mitindo ya muziki wake kutegemeana na wakati ama kutokana na aina ya wanamuziki walioipigia.

Ingawaje mpaka sasa Watanzania wenye vimelea vya muziki wanaendelea kupata ladha ya muziki wa Jamhuri ya Congo DR kupitia bendi kama vile, FM Academia, Tukuyu Bend, Mashujaa Musica na nyinginezo, lakini haiyumkini huenda viwango vya bendi hizo bado havijaweza kukidhi matakwa na haja za wapenzi hao, achilia mbali kutofikia mafanikio ama umaarufu uliokuwa umetamalaki ndani ya bendi za Marquiz na Safari Sound.

Nimejikita kuzungumzia zaidi bendi za OMACO na OSS, kwa kuwa hata 'vijana' wa wakati huo, (wanaweza kukubaliana na mimi) kuwa, ilikuwa ni vigumu kwao kupata usingizi pasipo kwenda kucheza muziki wa Wacongo ambao baadhi yao, waliamua 'kuzamia' jumla nchini ilhali wengine wakiamua kuoa wanawake wa Kitanzania ambao walionyesha kuvutiwa mno na miziki ya kikwao.

Hata hivyo wakati unasoma makala haya, ni vyema kujua kwamba historia ya muziki wa Tanzania inaendelea kubebwa kwa asilimia 90 na bendi za kizalendo za Orchestra Mlimani Park 'Sikinde Ngoma ya Ukae' na iliyokuwa OTTU Jazz ambayo sasa inajulikana kama Msondo Ngoma ambazo bado zinang'ara hadi hivi leo.




Marehemu Kasongo Mpinda (kushoto) na King Kiki.

Bendi hizo mbili hasimu ambazo zingali zinaendelea 'kupeta', zikiwa zimejiwekea misimamo imara ya kutoyumbishwa na mageuzi ya kufuata mirindimo ya muziki wa Kicongo, ndizo zinaaminika kuwa bado ni alama halisi na kielelezo tosha cha muziki halisi wa Kitanzania.

Kutokana na kinachodaiwa kuandamwa na ukata, bendi nyingi za kizalendo, zinadaiwa kupoteza sifa na mvuto kwa wapenzi huku nyingine zikiripotiwa kufa kibudu kutokana na nyingi kati yake kujikita kupiga zaidi muziki kwa kutegemea kiingilio cha kinywaji badala ya kutoza fedha mlangoni.

Bendi ya Orchestra Marquiz du Zaire iliyokuwa imesheheni 'majembe' ya kazi enzi hizo (kwa maana ya kuwa na wanamuziki wakali na wenye uwezo mkubwa wa kupiga muziki), iliingia nchini mwaka 1972 ikiwa inajulikana kwa jina la Super Gadi Jazz.


Nguza Viking

Madhumuni ya bendi hiyo yalikuwa ni kwenda nchini Uganda kwa nia ya kutoa burudani; huku ikiwa imeazimia kuweka maskani yake katika jiji la Kampala.

Hata hivyo, 'Pedeshee' wa wakati huo, Issa Batenga, alizima mpango huo kwa kuwa alifanya umafia wa 'kuiba' wanamuziki wote wa bendi hiyo, hivyo kujikuta wakilazimika kusimika maskani yao eneo la Tazara (yalipo makao makuu ya kiwanda cha Bakheresa), ilhali ukumbi uliokuwa ukitumiwa na bendi hiyo, ukiitwa Mikumi Tours Park.

Bendi hiyo baadaye ilikuja kuwa na nguvu ya kiuchumi ikiwa inamiliki vitegauchumi kama vile mashamba yenye matunda, nyumba na matrekta, ilikuwa na sura za wanamuziki waliotikisa wakiwa chini ya uongozi wake, marehemu Chinyama Chiyaza 'Chichi'.

Mbali na 'Chichi', listi ya wanamuziki wengine wa bendi hiyo walikuwa ni Mbuya Makonga 'Adios', Vicky Numbi Nguza, Kanku Kelly Kashama, Mukumbule Lolembo 'Parashi', Mutombo Lufungula 'Audax', Chibangu Katayi, Mzee Tito Paul, Mpoyo Kalenga na Totoo Nyoma Mwamba.

Wengine ni Ilunga Banza Mchafu, Mulenga Kalonji 'Vata', Mafumu Bilali 'Bombenga', Mbombo wa Mbomboka, Ilunga Ngoi, Kayembe Ndalambu, Mutombo Sozi, mnenguaji Mcongo, Ngalula Chandanda na gwiji Kikumbi Mwanza Mpango 'King Kikii' ambaye hata hivyo, aliingia na kutoa mguu kabla ya kuchomokea bendi ya OSS.

Wana Marquiz enzi hizo, ilikuwa imefanya usajili wa 'kufa mtu' kila idara. Kwani ili kujihakikishia 'inazitesa' bendi nyingine, hasa zile zilizokuwa zimepania kushindana nayo; miaka michache baadaye iliwaongeza kundini wakali wengine wakiwemo, Athuman Majengo, Abdallah Kimeza, Hatibu Iteitei na Mukuna wa Mukuna 'Roy'.

Mwaka 1985 bendi hiyo ilipata pigo baada ya kiongozi wake, Chinyama Chiyaza kufariki dunia; hivyo kufanya mikoba ya uongozi ikabidhiwe kwa mpiga gita la solo, Nguza Chibangu aliyebadilisha majina ya mitindo kutoka 'Kamanyola bila jasho', 'Sendema ya moto' kisha kuingiza mtindo mpya wa 'Ogelea piga mbizi'.

Mwaka 1986 bendi hiyo ikiwa na sura za wanamuziki wapya, Tshimanga Kalala Assosa, Kasaloo Kyanga na pacha wake Kyanga Songa, Issa Nundu, Kasongo Mpinda 'Craytone' na wengineo, bendi hiyo ilihamisha mabegi na kwenda kujikita Ukumbi wa White House, Ubungo.

Ukumbi huo ulikuwa ukimilikiwa na Mzee Camelius Jerome Mosha, baba mzazi wa Mtangazaji, marehemu Fred Mosha 'Chimbachimba'.

Itaendelea Uk. 21.

# Usiku ulikuwa mfupi enzi za Marquiz, OSS




Hassan Rehani Bitchuka (kulia) na marehemu Shaban Dede

Inatoka Uk. 20.

Miongoni mwa nyimbo za awali zilizoipa chati bendi hiyo, wimbo wa 'Mobali Malolee' ndiyo ulikuwa kwanza kutungwa, ukifuatiwa na nyimbo nyingine za 'Feda Mtoto wa Lubumbashi', 'Nunuu' pamoja na 'Mongo Liwaa'.

Licha ya umwamba wa bendi ya OMACO kutunga utitiri wa nyimbo nyingi zilizowavutia wapenzi wengi na wa kila rika, bendi hiyo ilipata kigingi cha upinzani kutoka kwa miamba, Orchestra Safari Sound ambayo baada ya kuanzishwa na tajiri mmoja Mtanzania, Huggo Kisima Desemba 1978, ilitokea kuwa moto wa kuotea mbali.

Tajiri huyo alimpa jukumu la kuiongoza OSS mwimbaji Mbombo wa Mbomboka huku bendi hiyo iliyoweka maskani katika vilima tulivu vya Safari Resort, Kimara ikianza kupiga muziki wake kwa kutumia mtindo wa 'Nyekese Paralizee'.

Mbomboka kama ilivyo ada ya Wacongo, naye alikusanya rundo la Wacongomani wenzake, nia ikiwa ni kuimarisha OSS ili iweze kumudu ushindani na bendi ya Marquiz du Zaire ambayo ilikuwa haishikiki.

Kiongozi huyo aliwaita mastaa, Dingtuka Molay 'Nyama ya nyani', Kababa Nkomba, Chibanda Soni, Hembi Frolee, Sammy Makaza, Yusuph Kaloya, Ramadhani Mtono kisha miaka saba baadaye, OMACO iliwaleta waimbaji wawili wenye asili ya DRC, Bobo Sukari na Fred Butamu ambao waliing'arisha maradufu.

Ushindani wa bendi hizo zilizokuwa zinasababisha wapenzi kutolala usiku, hususan siku za wikiendi, ulizidi kuwa mkali baada ya tajiri Kisima (Huggo), kumpa fungu la fedha Mbombo ili aongeze wanamuziki wengine wakali.

Mwaka 1979, Mbomboka 'alishusha nondo' nyingine mpya ndani ya OSS ambapo wanamuziki Kabeya Badu, Kasongo Otrish, Kadesi Rugambwa, Kalala Mbwembwe, Akulyake King Maluu na Nkulukutu Motoo wa Bandoki ambao kwa pamoja waliifanya bendi hiyo iwe ya kuogopwa.

Hata hivyo, uongozi wa OSS haukuridhika na ujio wa wanamuziki waliokuwepo, bali mwaka 1986 bendi hiyo ilifanya 'surprise' (tukio lisilo la kawaida), ambapo iliibomoa bendi iliyokuwa ikitisha (wakati huo), ya Orchestra Mlimani Park 'Sikinde' kwa kunyakua mastaa wake saba kwa mpigo.

Miongoni mwa wanamuziki wenye majina makubwa ambao OSS 'iliwachomoa' kwa njia ya umafia kutoka 'Sikinde' ni gwiji, marehemu Muhidin Gurumo, Hassan Bitchuka, marehemu Kassim Rashid 'Kizunga', marehemu Chipembele Said 'Bob Chipe', marehemu Abel Balthazar, marehemu Charles John 'Ngosha' na marehemu Ally Makunguru.

Mpiga gita la solo wa kutegemewa wa bendi ya Mlimani Park, Michael Bilali katika sakata hilo, alifichwa na viongozi wake azma ikiwa ni kutoidhoofisha.

Bendi ya OSS ilifia mikononi mwa mpiga gita la nyuzi 12, (nyuzi dazani), marehemu Fred Ndala Kasheba 'Supreme' mwishoni mwa miaka ya 98, ilizoa umaarufu mkubwa ikiwa inatumia mitindo ya 'Chunusi' na 'Dukuduku' ambayo itakumbukwa daima.

Hata hivyo, bendi hiyo ilibadili staili ya kuachana na kasumba ya kuajiri wanamuziki wa DRC baadaye, ilijijenga kwa kuajiri 'masupastaa' kama vile, Benovilla Anthony Magali, Twahir Mohammed, Monga Stanley, Mbaraka Othuman 'Muba' ambao waliiweka kwenye medani ya juu wakiwa wanatumia mitindo ya 'Power Iranda' na kisha 'Rashikanda Wasaa'.

Hata hivyo, kituko cha kufurahisha ni kwa mpiga gita la ridhimu, Abdallah Gama 'String Master' ambaye licha ya 'kunusa' raha zilikuweko 'Ndekule' kwa wiki moja, mkongwe huyo aliamua kurejea 'Sikinde' hata kabla ya wiki moja haijakatika.

Bendi ya OSS iliyojipatia sifa kedekede kutokana na tungo za nyimbo zake kuwa zenye kusisimua, ilipitia mikononi mwa viongozi kadhaa ambao ni pamoja na Benovilla Magali maarufu 'Kingalu', ambaye aliwaongoza wazalendo wenzake akiwa anatambia mtindo wake wa 'Rashikanda Wasaa'.

Kabla ya hapo, OSS ilipiga muziki wake kwa kuitumia mitindo ya 'Masantula Ngoma ya Mpwita' ulioasisiwa na King Kiki, 'Dukuduku' wa hayati Kasheba na 'Ndekule' wa Mzee Gurumo. Mitindo hiyo inaendelea kuwa ni gumzo la nchi hadi leo.

Ukiachana na wababe hao wawili wa muziki kutoka Jamhuri ya RDC kuteka soko la muziki wa Tanzania kwa muda mrefu, upande mwingine 'waumini' wa muziki chini, ulikuwa huwaambii kitu kwa kuzihusudu bendi za Kizalendo.

Miongoni mwa bendi zilizotajwa kuvunja baadhi ya ndoa ni Vijana Jazz 'Sagarumba', Washirika 'Njatanjata', Tabora Jazz 'Segere Matata', Tancut Almasi 'Wana Kinye Kisonzo Fimbo Lugoda', Super Matimila na Mwenge Jazz 'Paselepa' ambazo wafuatiliaji wa mambo wanadai, wakati huo wasingekubali kulala pasipo kucheza muziki wake.

Kurejea kwa Maquiz iwe chachu ya kufufuliwa kwa bendi nyingine zilizotikisa hapa nchini ili muziki huu wa dansi urudi kwa kishindo kama enzi zake badala ya kuwaachia Wana-Bongofleva wakitamba hivi sasa bila upinzani wowote ule.

**Kwa maoni na ushauri; 0768 888 787 ama 0784 122 020.**



Asha Baraka akiwa na marehemu Muhidin Gurumo

# Baadhi ya istilahi za Kiswahili katika mpira wa miguu - 2

**Na Richard Mtambi**

**Inaendelea kutoka wiki iliyopita:**

Aidha, kuna viungo wa ushambuliaji ambao tumezoea kusikia wakiitwa attacking midfielders kwa lugha ya Kiingereza.

Kila timu iwapo uwanjani katika mpira wa miguu huwa na kiongozi wa wachezaji. Huyu, aghalabu huvaa kitambaa katika mkono wake wa kulia karibu na bega. Istilahi ya lugha ya Kiingereza inayotumiwa kumwita ni captain/team captain.

Katika lugha ya Kiswahili kuna visawe viwili ambavyo vinaweza kutumika kumuita; cha kwanza ni cha utohozi kutoka katika lugha ya Kiingereza, yaani, kapteni/kapteni wa timu lakini kisawe cha pili katika lugha ya Kiswahili ambacho nacho kina asili ya lugha ya kiarabu ni nahodha/nahodha wa timu.

Baadhi ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili ambao husisitiza sana utumiaji wa maneno yenye asili ya lugha za Kibantu badala ya haya ya utohozi wanashauri matumizi ya jina kiranja/kiranja wa Timu.

Kiranja, kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili, Toleo la Pili iliyochapishwa mwaka 2017, (Uk. 481) iliyoandikwa na BAKITA, ni: a. kiongozi wa kikundi fulani b. kijana anayewasimamia wengine darasani au shuleni ch. Kijana anayekuwa wa kwanza kutahiriwa miongoni mwa vijana walioandaliwa kuingia jandoni.



Watangazaji wa Azam TV, Gharib Mzinga (kulia) na James Samwel




Mtangazaji wa TBC FM, Nazareth Upete

Kwa kuangalia maana za kiranja zilizotolewa ni dhahiri kuwa maana ya a., ingeweza kusadifu kuwa jina la kiongozi huyu wa wachezaji wenzake kiwanjani.

Hata hivyo, ukopaji na utohozi ni tabia ya kila lugha kuongeza msamiati wake, kwani hakuna lugha inayojitosheleza na hakuna lugha ambayo haina maneno kutoka katika lugha nyingine.

Aidha, katika usanifishaji, aghalabu wasanifishaji huzingatia maoni ya wazungumzaji ambapo baadhi ya maneno yenye mashiko katika uga fulani wa matumizi husanifishwa na kuwa maneno ya Kiswahli sanifu.

Kwa kawaida mchezo wa mpira wa miguu aghalabu huchezwa kwa dakika 90, yaani, dakika 45, kipindi cha kwanza (first half) na kisha dakika 45 nyingine za kipindi cha pili (second half).

Baada ya dakika arobaini na tano za kipindi cha kwanza huwa kuna muda wa takribani dakika 15 kwa ajili ya kupumzika. Istilahi ya Kiswahili ya kuashiria kipindi hiki cha kupumzika ni mapumziko ilhali kwa Kiingereza ni half time.

Aidha, kabla ya kumalizika kwa kipindi chochote kati ya vipindi hivi viwili vilivyotajwa, huwa kunakuwa na muda wa kufidia mpira uliposimama kutokana na sababu mbalimbali.

Istilahi ya Kiswahili ya muda huu ni muda wa nyongeza, baadhi huita dakika za majeruhi ambapo wanaopenda kutumia istilahi za kiingereza huuita muda huu extra time.

Mpira unapomalizika istilahi yake ya Kiswahili ni mwisho wa mchezo ambapo wengi wetu tumezoea kusikia full time.

Vilevile, kwa mchezo wa mpira wa miguu ambao mshindi wake hapatikana baada ya dakika tisini za kawaida na katika mazingira ya kuhitajika kupatikana kwa mshindi, muda wa kucheza huongezwa aghalabu kwa dakika thelathini.

Muda huu ambao kwa Kiingereza huitwa extra period/extra time, kwa lugha yetu adhimu ya kiswahili kisawe chake ni kipindi cha nyongeza/muda wa nyongeza.

Istilahi nyingine katika mchezo huu ni zile zinazoelezea timu ipi iko nyumbani na timu ipi iko ugenini. Pamoja na kuwapo kwa istilahi za Kiswahili katika mazingira haya lakini aghalabu utawasikia watangazaji na wachambuzi wakitumia maneno home team badala ya timu mwenyeji/timu ya nyumbani na visiting team badala ya timu ngeni/ timu ya wageni.

Neno lingine linalotumika sana siku hizi ni assist ambayo inapaswa kuwa pasi ya mwisho iliyozaa goli.

Tuhitimishe kwa kuorodhesha baadhi ya Istilahi za Kiswahili za Mpira wa Miguu na kuonesha visawe vyake vya Kiingereza katika mabano: kona (corner), kuotea/kuzidi (off - side), mchezaji wa kulipwa (professional player), meneja wa timu (team manager), mwamba wa goli (cross bar), klabu ya soka/klabu ya mpira wa miguu (football club), mstari wa goli (goal line), nguzo ya goli (goal post), wavu/nyavu (net/nets), mchezaji wa akiba (substitute), n.k.

Tuwatanabahishe wapendwa wasomaji wetu kwamba Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) lina kitabu chake cha Istilahi zaKiswahili. Kitabu hiki kina msamiati unaotumiwa katika fani mbalimbali. Moja ya uga ambao istilahi zake zimo ni uga wa michezo.

Aidha, BAKITA, litaendelea kuandika kamusi za fani mbalimbali ikiwamo michezo kwa lengo la kuendelea kutoa istilahi zitakazotumiwa na wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili.

Hivyo, tunawashauri watangazaji, waandishi na wachambuzi wa michezo, hususani Mpira wa Miguu kutumia istilahi hizi na pia kuwasiliana na wataalamu wa BAKITA pindi wanapopata matatizo au kutaka ufafanuzi wa usahihi wa matumizi ya istilahi za michezo.

Hii ni kwa sababu kuwa BAKITA pia, lina wajibu wa kushirikiana na mashirika, asasi na watu binafsi, kufuatilia, kushauri na kusimamia shughuli zinazolenga kukuza Kiswahili.

Mpira wa Miguu na Michezo kwa ujumla, ni moja ya nyanja ambazo zinaendeleza matumizi ya lugha ya Kiswahili kitaifa na kimataifa.

Tujivunie Kiswahili!

**Mwandishi wa makala haya ni Mhariri Mkuu wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Mawasiliano yake ni 0713 – 616 421.**

## Kona ya Urembo



# Mwonekano na urembo kwa Bi. harusi

**Na Hidaya Machupa**

MWONEKANO wa bi harusi katika urembo na mitindo ambao mara nyingi huangazia mitindo mipya ya mavazi, mapambo ya uso, nywele, na mwenendo wa jumla katika harusi.

Bi. harusi wanatafuta mwonekano unaojumuisha uzuri wa kisasa na wa kitamaduni. Hapa kuna baadhi ya mwelekeo unaojadiliwa katika makala bora za urembo na mitindo ya bi harusi.

Mavazi ya Bi. harusi yanaendelea kuwa ya kifahari, yakijumuisha vitambaa vya hariri, lace, na satin. Wabunifu wengi wanachanganya vipengele vya kisasa na vya kihistoria, kama vile mabega yaliyo wazi mitindo ya mavazi ya miaka ya 1920, au mavazi yenye mikia mrefu.

Kuna mwelekeo unaozidi kuwa maarufu wa mavazi yenye miundo rahisi, bila mapambo mengi, lakini yenye mvuto wa hali ya juu. Haya mavazi mara nyingi huja na ufundi mzuri na vipande vidogo vya mapambo vinavyoongeza uzuri wa asili.

Bi. harusi wengi wanapendelea mapambo mepesi yanayoakisi uzuri wa asili, yakilenga kutoa ngozi yenye mng'ao na afya. Rangi za waridi, 'peach', na 'nude' ni maarufu kwa midomo, huku macho yakipambwa kwa vivuli vya dhahabu au shaba.

Mapambo ya kuifanya ngozi ionekane yenye kung'aa yamekuwa maarufu sana. Wataalam wa urembo wanatumia 'seramu' zenye unyevu, viangazaji na poda zinazofanya ngozi ing'ae kwa namna ya asili.

Mitindo ya nywele yenye mwonekano wa asili, kama vile nywele zilizolegezwa na mawimbi ya asili au zilizokusanywa nusu juu na nusu chini, imekuwa maarufu sana.

Bi.harusi wengi wanarejea mitindo ya nywele ya miaka ya zamani kama vile vibanio vya maua, vibanio vya lulu, au headpieces za vintage ili kuongeza uzuri wa kihistoria kwenye harusi zao.

Vifuniko vya nywele, kama vile veils fupi na ndefu, zimeendelea kuwa maarufu, zikiwa zimechaguliwa kulingana na urefu wa mavazi. Veils ndefu zinazofikia chini zimekuwa zikivutia zaidi kwa bi harusi wanaopendelea mwonekano wa kifalme.

Lulu, dhahabu, na maua ya bandia vinatumika kama pambo la nywele kuongeza uzuri wa mwonekano wa bi harusi, hasa kwa wale wanaopendelea kuacha nywele huru au kufanya mitindo ya up-do.

Wengi wanapendelea kuonyesha urithi na tamaduni zao kupitia mavazi ya harusi ya kitamaduni, kama vile vazi la 'saree' kwa Wahindi au kanzu kwa wapwani, huku yakichanganywa na vipengele vya kisasa kama vile rangi za kupendeza na mapambo ya kifahari.







### HINA NA MITINDO YA MAPAMBO YA KAWAIDA

Bi. harusi wa asili ya Kiarabu, Hindi, na Afrika wanaendelea na mila ya kutumia hina yenye michoro mizuri ya kiasili mikononi na miguuni.

Jamii mara nyingi ina maoni yenye nguvu kuhusu mwonekano wa Bi. harusi kwa sababu harusi ni tukio la kijamii linalobeba umuhimu mkubwa katika tamaduni nyingi.

### KUUTATHMINI MWONEKANO WA BI HARUSI

Uzuri wa kitamaduni, desturi sambamba na kuheshimu mila katika tamaduni nyingi, mwonekano wa Bi. harusi unahusiana moja kwa moja na mila na desturi.

Watu wanatarajia Bi. harusi avae mavazi yanayozingatia tamaduni za eneo hilo, kama vile vazi la 'saree' kwa Wahindi, kanzu na joho kwa wapwani, au gauni la harusi la jadi kwa Wazungu.

Mwonekano unaojumuisha mavazi ya kitamaduni unachukuliwa kama njia ya kuheshimu urithi wa familia na jamii.

### RANGI ZA KIPEKEE

Rangi pia ina maana kubwa. Kwa mfano, nyeupe ni maarufu kwa bi harusi wa Kimagharibi kuashiria usafi, wakati rangi kama nyekundu au dhahabu ni za kawaida kwa harusi za Wahindi au za Kiarabu, zikiwa zinaashiria furaha na ustawi.

Jamii inaweza kutoa maoni mazuri au ya kushutumu kulingana na uchaguzi wa rangi ya vazi la Bi. harusi.

### SAUTI ZA KISASA KUHUSU MWONEKANO

Katika miaka ya hivi karibuni, jamii imeanza pia kusisitiza umuhimu wa Bi. harusi kuhifadhi urembo wa asili badala ya kutumia mapambo ya kupita kiasi.

Kuna sauti zinazowakilisha mwelekeo wa "clean beauty" ambapo bi harusi anashauriwa kuepuka vipodozi vikubwa ili kujitokeza kwa uzuri.

Inashauriwa Bi. harusi asizidiwe vazi na msimamizi wake kwa sababu harusi ni siku maalum kwa bi harusi, na anatarajiwa kuwa kitovu cha macho ya wageni. Kwa hivyo, mavazi ya bi harusi yanatakiwa kuwa ya kipekee, yenye mvuto zaidi na kuonyesha hadhi yake katika tukio hilo.

Bi. harusi anatarajiwa kuwa katikati ya tukio hilo. Vazi lake linapaswa kuwa na uzito wa kipekee ili kumtofautisha na watu wengine, hasa msimamizi wake. Ikiwa msimamizi atazidi kwa urembo au uzuri wa mavazi, anaweza kuondoa usikivu unaostahili kwenda kwa bi harusi.

Kwa hiyo, ushauri huu unalenga kuhakikisha kwamba Bi. harusi anapata heshima inayostahili katika tukio lake maalum, na msimamizi wake anashirikiana kwa njia nzuri katika kuifanya siku hiyo kuwa ya kipekee bila kuleta ushindani wa kimwonekano.

Leo yetu ndiyo kesho yetu

Uelekeo Spoti

| Jumatano Oktoba 23-29, 2024 |

## Hamduni: Tumeziona changamoto za dabi

**Na Mwandishi Wetu**



MWENYEKITI wa Kamati ya Waamuzi ya TFF, Nasoro Hamduni amesema changamoto za maamuzi yaliyotokea katika mechi ya watani wa jadi Simba na Yanga wameyaona na wanasubiri vyombo vya maamuzi vitakavyoamua.

Akiongea kupitia Kituo kimoja cha Redio, Hamduni mwamuzi wa zamani wa kimataifa amesema kuwa, yeye na Kamati yake walipanga waamuzi hao kuchezesha mechi hiyo na yaliyotokea wameyaona na wanasubiri mamlaka zinazohusika kutoa taarifa.

"Changamoto zipo, wachezaji wana changamoto, waamuzi wana changamoto, sisi viongozi tuna changamoto na hata nyie vyombo vya habari mna changamoto; hivyo tuache kuendeleza taharuki," amenena Hamduni.

## Manura arejeshwa Taifa Stars, kocha ni Shime

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Bakari Shime amekabidhiwa mikoba ya timu ya taifa, Taifa Stars, kitachopambana na Sudan kwenye mechi mbili za kusaka tiketi ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wanaocheza Afrika na bila kusita kocha huyo amemrejesha kipa, Aishi Manura 'Tanzania One' kikosini.

Wachezaji wengine waliotwa kwenye kikosi hicho ni pamoja na Isaya Kasanga kutoka TFF Academy, Anthony Mpemba (Azam FC), Paschal Msindo (Azam FC), David Braison (JKT Tanzania), Nickson Mosha (KMC), Lameck Lawi (Coastal Union), Adbulrahim Bausi (JKT Tanzania) na Vedastus Masinde (TMA FC).

Kocha Shime pia amewaita Ibrahim Ame toka Mashujaa FC, Hiija Shamte (Kagera Sugar), Adolf Mtasigwa (Azam FC), Abdulkarim Kiswanya Azam FC), Charles Semfuko (Coastal Union), Shekhan Hamis (Yanga), Ahmed Pipino (Magnet FC) na Sabri Kondo (KVZ).

Pia wamo Salumu Ramadhan KenGold), Ismail Kader JKT Tanzania), Bakari Msimu Coastal Union), William Edgar (Fountain Gate FC), Seleman Mwalimu (Fountain Gate FC). Valentino Mashaka (Simba) na Cyprian Ngushi wa Mashujaa FC.





# Yanga imeshindikana

## ● Yajipigia kila anayekatiza mbele yao



**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya NBC, Yanga wamejipatia ushindi wa sita katika mechi sita mfululizo baada ya kuibamiza JKT Tanzania bao 2-0.

Kwa ushindi huo, Yanga wamejikusanyia alama 18, magoli 11 ya kufunga huku hawajaruhusu wavu wao kutikiswa hadi sasa.

Yanga kama kawaida walianza kipindi cha kwanza kwa kuelekezwa mashambulizi mfululizo kwenye lango la JKT Tanzania, lakini walikutana na ukuta wa wachezaji wengi wa wapinzani wao.

JKT walianza walianza kwa kuwaheshimu Yanga, kwa kuwaacha wacheze mpira huku wao wakijilinda kwa kujaza wachezaji wengi nyuma 'low brock'.

Mashambulizi hayo mfululizo ya Yanga hatimaye yaliwashinda JKT na dakika ya 22 wakakubali yaishe baada ya Pacome Zouazoa kuifungia timu yake bao la utangulizi kufuatia pande maridhawa la Clatous Chama.

Baada ya kupata bao hilo, Yanga ilipunguza kasi yake ya mashambulizi na kufanya mpira kuchezwa katikati ya uwanja.

Dakika ya 39 ya mchezo kipa wa JKT Tanzania, Denis Richard alipigwa kadi nyekundu ya kujitakia baada ya kudaka mpira nje ya eneo la mita 18.

Adhabu hiyo aliyosababisha kipa Denis ilitumiwa vizuri na Yanga kujiandikia bao la pili kupitia Chama dakika ya 42.

Kama ilivyokuwa kipindi cha kwanza, Yanga ilianza kipindi cha pili kwa kasi na mashambulizi mfululizo kwenye lango la JKT lakini hawakufanikiwa kupata bao la mapema kwenye kipindi hiki.

Mudathiri Yahya Abasi aliyeingia kipindi cha pili nusura aipatie Yanga bao la tatu dakika ya 59 lakini shuti lake la mbali lilipanguliwa na kipa Omari Gonzo na kuwa kona tasa.

JKT pamoja na kuwa pungufu kuna nyakati katika kipindi hiki cha pili walikuwa wanacheza soka safi na nusura dakika ya 77 wapate goli kama si papara za mshambuliaji wao Mohamed Bakari kushindwa kufunga akiwa yeye na kipa wa Yanga, Djigui Diarra.

# Simba yazindukia kwa Prisons

**Na Mwandishi Wetu**



BAADA ya kushindwa kufanya vizuri katika mechi mbili zilizopita, hatimaye Simba imekwenda kuzindukia Mbeya kufuatia kuichapa Prisons bao 1-0.

Simba ilianza kusaka ushindi mapema kipindi cha kwanza na juhudi zao zilizaa matunda dakika tano ya mchezo lililowekwa kimiani na beki wao, Che Malone Ponda.

Goli hilo lilikuwa kosa la kipa wa Prisons, Mussa Mbisa aliyeshindwa kuudhibiti vema mpira wa adhabu uliopigwa na Kibu Denis na Malone akafunga bao rahisi kabisa.

Baada ya hapo mpira ulichezwa zaidi eneo la katikati ya uwanja, huku kukiwa na mashambulizi machach yule.

yaliyofika kwenye milango ya timu zote mbili.

Kipindi cha pili Simba walirudi na moto mkubwa lakini walishindwa kuzitumia vema nafasi mbili waliotengeneza ndani ya dakika tano za mwanzo za kipindi hicho.

Dakika ya 56 Simba ilifanya shambulizi zuri kwa kiungo Fabrice Ngoma kupiga pasi ndefu kwa Kapombe ambaye naye alipiga krosi murua, lakini Leonel Ateba alishindwa kufunga bao.

Dakika moja baadaye Ateba alishindwa tena kutumia vema pasi ndefu ya Ngoma.

Dakika ya 60 kipa wa Simba, Moussa Camara aliumia baada ya jitihada kubwa aliyoifanya kuokoa shambulizi kali la Tanzania Prisons.

Kipa Mbisa aliiokoa Prisons kufungwa bao la pili baada ya kupangua vizuri kichwa cha Steven Mukwala aliyeunganisha mpira wa adhabu uliopigwa Joshua Mutale.

Hadi mwamuzi Amina Kiando anapuliza filimbi ya mwisho, Simba 1, Prisons 0.